
# BWANA WETU NA KANISA LAKE

## (MWALIMU)



MAFUNDISHO YA BIBLIA KWA VIJANA WA AFRIKA

# BWANA WETU NA KANISA LAKE

Kimeandikwa na Jill B. Branyon

## MAFUNDISHO YA BIBLIA KWA VIJANA WA AFRICA

Africa Coordinated Curriculum
for Bible Study

Y5 - 3Ts

Used by permission of
International Publications Services

Published and Printed by
BAPTIST PUBLICATIONS HOUSE
Thika Road, Ruaraka
BOX 30370, NAIROBI

©

Copyright, 1986
Baptist Publications House
All rights reserved

## YALIYOMO

SURA UKURASA


1. Kristo Ni Bwana .............................. 7
2. Kristo Ndiye Msingi .......................... 11
3. Kuwa Shahidi ................................ 15
4. Kanisa Hapo Mwanzo .......................... 20
5. Kuongozwa na Roho ........................... 25
6. Tu Mmoja Ingawa Wengi ....................... 30
7. Tumechaguliwa Kwa Njia ya Kristo ............ 35
8. Kristo ni Kichwa cha Kanisa ................. 39
9. Tumeumbwa Tena Kwa Kusudi ................... 44
10. Jamaa ya Mungu ............................. 49
11. Kanisa Katika Mpango wa Milele ............. 54
12. Maombi ya Paulo kwa Kanisa ................. 59
13. Tukue Kwa Mfano wa Yesu .................... 64

## HABARI ZA MWANDISHI

Jill Beatty Branyon, mwandishi wa kitabu hiki ni mwalimu huko Nyeri Baptist High School, Nyeri, Kenya. Kabla ya kuja Kenya, alikuwa pia akiwafundisha wanafunzi wa high school huko Amerika.

Ametoka South Carolina huko Amerika. Alihitimu katika Winthrop College na University of South Carolina. Pia alihudhuria masomo katika seminari, Southwestern Baptist Theological Seminary.

Anasema kuwa hupenda sana wanafunzi, kupiga gitaa, kazi za mikono kama kushona na kucheza mpira wa kikapu. Anahudhuria katika Kanisa la Kibatisti huko Nyeri.

## SURA YA KWANZA
# KRISTO NI BWANA

### KUJITAYARISHA KUFUNDISHA

Somo Kutoka: Wakolosai 1:1-20

Vifungu vya Leo: Wakolosai 1:9-20

**Kifungu cha Kukumbuka**

> "Naye ndiye kichwa cha mwili, yaani, cha kanisa; naye ni mwanzo, ni mzaliwa wa kwanza katika wafu, ili kwamba awe mtangulizi katika yote" (Wakolosai 1:18).

Kusudi la Somo Hili: Ili niwafundishe wanafunzi wangu kuwa Yesu ni Mwokozi, Bwana na Mkuu wa kanisa.

Vitu vya Kusaidia Kufundisha: Uwe na ubao au karatasi kubwa ya kuandika maswali yatakayoulizwa katika somo.

**Msingi wa Somo Hili**

Katika sehemu hii tutajifunza msingi wa ukweli kuhusu kanisa. Tutaelewa kanisa ni nini, nani analiongoza kanisa, kanisa linavyofanya kazi yake na wajibu wa kila mmoja katika kanisa. Utapata kuelewa furaha na wajibu wa kuwa mshiriki wa kanisa.

Kitabu cha Wakolosai kimeandikwa na Paulo kwa kanisa lililokuweko huko Kolosai. Yeye mwenyewe binafsi hakuwafahamu waamini hawa, lakini alikuwa amepata habari zao labda kutoka kwa Epafura ambaye alifanya kazi kubwa katika kuliendeleza kanisa hilo. Barua hii iliandikwa wakati Paulo alipokuwa gerezani huko Roma.

Paulo alikuwa akiyaeleza matatizo katika kanisa. Kulikuwepo na mawazo na matendo ambayo hayakuwa

sehemu ya mafundisho ya Kristo. Waamini hawa walikuwa wamechanganya dini za asili na imani ya Kiyahudi na kuanza kuabudu malaika (Wakolosai 2:18) na mambo ya tohara (Wakolosai 2:11). Kwa vyo vyote, kutahiriwa kama mila ni kitu kinachofanywa na wengi, lakini kisiwe ni cha lazima ili mmoja awe mshiriki wa kanisa kama ilivyokuwa kule Kolosai.

Paulo alilieleza kanisa wazi kuwa Kristo pekee atosha kwa mtu kuwa mshiriki wa kanisa.

Unapoanza kusoma maandiko ya somo hili, angalia kifungu cha 9 kina maana ya kifungu cha 4 pale watu wa Kolosai walipokuwa washiriki kwa imani katika Yesu Kristo na upendo walioonyesha kwa waamini wengine. Angalia Yohana 13:35.

Nafasi ya kwanza ya Yesu katika kanisa ni kuwa yeye ni Mwokozi. Yesu aliliokoa kanisa. Alitoa uhai wake kuweka njia kwetu ya kuingia kanisani. Katika Yohana 14:6, Yesu anasema yeye ndiye njia pekee ya kwenda kwa Baba.

Tena katika Wakolosai 1:13-14 Paulo anasisitiza kuwa wokovu ni kwa njia ya Yesu tu. "Naye (Mungu)...akatuhamisha na kutuingiza katika ufalme wa Mwana (Yesu)...ambaye katika yeye tuna ukombozi, yaani, msamaha wa dhambi."

Pili, Paulo anaeleza kuwa Kristo ndiye kichwa cha kanisa. Sisi kama washiriki tunapaswa kufanya yale tunayoongozwa na Roho Mtakatifu. Maagizo tunayopokea kutoka kwa Kristo ni maneno yake kutoka katika Biblia na kwa kuomba, tuongozwe. Bwana atayasikia maombi yetu kama tutakuja kwake tukiwa tayari kufanya mapenzi yake.

Mwishoni Paulo anaeleza kuwa Kristo ni Bwana wa kanisa. Sehemu ya mwisho ya kifungu cha 18 inasema, "...ili kwamba awe mtangulizi katika yote." Yesu ndiye Bwana, chanzo cha

ibada na mambo yote ya kanisa. Msingi wa mikutano yote ya kanisa iwe katika Kristo pekee.

## KULIFUNDISHA SOMO HILI

### Utangulizi

Uliza: "Ni nani anayeliendesha kanisa letu?" Andika swali pamoja na majibu ubaoni. Baadhi ya majibu yaweza kuwa: ni mchungaji, wazee, Mungu, kiongozi wa kwaya na kadhalika. Mwanafunzi asome Wakolosai 1:18 na uliza swali hilo tena.

Uliza: "Je, mtu awezaje kujiunga na kanisa letu?" Andika swali pamoja na majibu ubaoni. Majibu yaweza kuwa: kwa kubatizwa, kwa kuongea na mchungaji, kumwamini Kristo na kwenda mbele ya kanisa. Mwanafunzi asome Wakolosai 1:4 na Wakolosai 1:13-14 na ulirudie swali tena.

Uliza: "Sehemu muhimu sana ya ibada ni ipi?" Liandike swali na majibu yake ubaoni. Mwanafunzi asome Wakolosai 1:18 na sisitiza sehemu ya mwisho ya kifungu hicho. Rudia tena swali.

Andika maneno haya ubaoni: Yesu ni Mwokozi, Bwana na Mkuu wa kanisa.

### Maelezo

Paulo alikuwa akiwaandikia watu wa Kolosai juu ya matatizo ambayo tunayo leo. Katika ushirika wao wa kanisa walikuwa wameongeza mambo mengi mazuri ya desturi.

"Kwa mfano, maandiko yanatuambia tuungame imani yetu mbele za watu, lakini desturi zetu ni kwenda mbele ya kanisa na kuungama mbele ya hao walioko. Ni tabia nzuri lakini je, ni ya kiroho? Kama wengine wakishindwa kufanya kama sisi tunavyofanya, je, watengwe kuwa washiriki wa kanisa?

"Paulo alisisitiza kuwa Yesu ndiye Mkuu wa kanisa. Licha ya hili, mara nyingi katika shughuli zetu na katika mikutano ya

kanisa tunatumia muda mwingi tukijadili mawazo yetu na tunashindwa kuyaomba mambo hayo. Hata vijana wakati mwingine hupanga mikutano na kufanya maandamano bila kufikiria kwanza kama mapenzi ya Mungu yanatimizwa katika hayo.

"Paulo alisisitiza kuwa Kristo ndiye Bwana wa kanisa. Mara nyingi tunaharakisha tu katika ibada zetu bila kufikiria ya kuwa Kristo yupo pamoja nasi. Tunaweza kuimba nyimbo zetu, tuombe na kutoa sadaka kwa Kristo peke yake. Kumwabudu Kristo kama Bwana ni kutoa nguvu na muda ili tumfurahishe yeye."

**Ukweli Katika Maisha Yetu**

"Ebu tutazame tena maswali yetu ya leo. 1. Je, mtu atajiungaje na kanisa letu? 2. Nani analiongoza kanisa letu? Ni kristo kwa njia ya Roho Mtakatifu. 3. Kitu muhimu sana kwetu cha kufanya katika ibada ni nini? Ni kumwabudu Kristo."

Waulize wanafunzi wataje njia ambazo wana hakika nazo kuwa Kristo anazitumia kuliongoza kanisa lao. (Kwa kuifuata Biblia na waombe kuongozwa) Waulize wanafunzi ni mambo yapi wanaweza kuyafikiria ya kumfuata Kristo wakati wa ibada.

Wanafunzi warudie na kukiandika kifungu cha kukumbuka.

**Kuomba**

1. Omba ili kila mwanafunzi aelewe kuwa imani katika Yesu Kristo ndiyo njia pekee ya kuwa mshiriki wa kanisa.

2. Omba kuwa kila mwanafunzi atakuwa mwaminifu na mshiriki anayewajibika kwa kanisa.

SURA YA PILI

# KRISTO NDIYE MSINGI

## KUJITAYARISHA KUFUNDISHA

Somo Kutoka: I Petro 2:4-8

Vifungu vya Leo: Mathayo 16:13-27

**Kifungu cha Kukumbuka**

> "...Mtu ye yote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake, anifuate" (Mathayo 16:24).

Kusudi la Somo Hili: Nifundishe kuwa Yesu ndiye msingi wa Kanisa na kila sehemu ya kanisa imejengwa juu yake.

Vitu vya Kusaidia Kufundisha: Ubao au juu ya karatasi kubwa andika: "Ni kitu gani kinacholifanya kanisa liwe tofauti na vikundi vingine vya watu au vyama?"

**Msingi wa Somo Hili**

Mathayo aliiandika Injili yake kwa Wayahudi wa siku zake na akajaribu kuwaonyesha kuwa Yesu alitimiza unabii kuhusu Masihi.

Tunapoyaangalia maandiko ya somo la leo, tuelewe kuwa kabla ya vifungu hivi (Mathayo 16:1-12) Yesu alikuwa na makutano ya kuchukiza na mafarisayo na pia wanafunzi wake mwenyewe hawakumwelewa.

Kwa hivyo, Yesu alipouliza, "Mwana wa Adamu ni nani?" Hii ilifuatwa na mawazo ya aina mbili yasiyo sahihi kumhusu yeye.

Yesu kila mara alijiita Mwana wa Adamu. Jina hili maana yake ni Masihi. Kama lilivyoandikwa katika Danieli 7:13-14

ambapo Mwana wa Adamu ndiye atakayetawala ufalme wake milele. Maono haya ya Mwana wa Adamu pia tunayakuta katika Ufunuo wa Yohana 1:13. Maana nyingine ya jina, Mwana wa Adamu kama Yesu alivyojiita linaonyesha kuwa wafuasi wake wanaelewa kuwa kweli alikuwa mwanadamu na akatoa uhai wake kwa wanadamu.

Yesu alipouliza swali mara ya pili, "Nanyi mwaninena mimi kuwa ni nani?" Alihitaji jibu la wazi.

Jibu la Petro ni msingi ambao kanisa limejengwa. "Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai." Hakuna ungamo jingine isipokuwa Yesu ndiye Kristo. Yohana 11:25-26 inatuambia kuwa ni lazima tumwamini yeye peke yake.

Yesu akajibu kwa furaha, "Heri wewe, Simoni Bar-yona!" Heri maana yake ni furahi. Thawabu ya jibu hili inatolewa na Baba aliye mbinguni. Pia tunaelewa .kuwa mtu hawezi kumfuata Yesu isipokuwa kwa njia ya Mungu akiitwa na Roho Mtakatifu.

Yesu akasema "...na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu..." (kifungu cha 18). Mwamba ni ungamo imara Petro alilotoa kuhusu Yesu. Yesu aliongeza kuwa milango ya kuzimu haitalishinda kanisa kwa sababu limejengwa juu ya ungamo kuwa Yesu ni Bwana. Amezishinda falme za giza kwa kufufuka kutoka kwa wafu, na amelipa kanisa nguvu za kuyashinda majeshi ya Shetani.

## KULIFUNDISHA SOMO HILI

### Utangulizi

Waulize wanafunzi: "Je, vijana wanamwelewaje Yesu? Wanasema yeye ni nani?" Sema: "Kuna mawazo mengi ya kupotosha kuhusu Yesu duniani siku hizi. Watu wengine wanafikiri kuwa habari za Yesu ni hadithi za kitabu cha zamani

sana, yaani Biblia. Wengine wanaona kuwa alikuwa mtu mzuri, na wanajaribu kuishi kwa kadiri ya amri zake. Wengine wanaamini kuwa yeye ni mmoja kati ya manabii wengi na kuwa yeye si tofauti na Mohamedi, Musa au Buddha. Lakini baadhi ya watu, wanaoitwa Wakristo, wanaelewa kuwa Yesu ni Mwana wa Mungu. Wakristo wanaamini kuwa Yesu alishiriki katika uumbaji (Soma Yohana 1:1.) na kuwa alikuja duniani ili autoe uhai wake kuwa kafara ya dhambi zetu. Wanaamini kuwa alilianzisha kanisa liwe kivutio cha dunia inayokufa.

"Kila mmoja wenu lazima amwelewe Yesu ni nani. Kusema tunamwamini tu Yesu haitoshi. Yakobo 2:19 inasema, '...Mashetani nao waamini na kutetemeka.' Wakristo wa kweli wanapaswa kumkubali mwenyewe kama Mwokozi na wajitoe kwa kazi yake hapa duniani kwa njia ya kanisa."

**Maelezo**

Sema: "Kuungama kwa Petro, 'Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai.' Ilikuwa ni zaidi ya maneno ya imani. Ebu tuangalie hili kwa undani zaidi. 'Wewe ndiwe Kristo' ina maana kuwa Yesu ametimiza ahadi zote walizopewa Wayahudi kuhusu kuja kwa Masihi. Kristo ni neno la Kigiriki lenye maana ya 'Masihi.' Yesu alikamilisha unabii wote. Wayahudi walikuwa wanamngojea Masihi wao. Walifahamu atatawala ufalme wake milele (Isaya 9:6), lakini hawakuelewa kuwa ufalme wake utakuwa huko mbinguni. Hawakuelewa kuwa atautimiza unabii wa aibu na kifo katika Isaya 53:1-6.

"Kuamini kuwa Yesu ni Kristo ni kuamini kuwa Yesu alitimiza ahadi na unabii kuhusu kifo na kufufuka kwake. (Angalia Zaburi 16:10; 110:1.)

"Pili kuseme kuwa Yesu ni Mwana wa Mungu aliye hai ni kuungama kuwa yeye mwenyewe ni Mungu. Yesu alikuwepo hapo mwanzo. Alikuja duniani kwa kusudi la kutuokoa.

Amepaa tena na yuko katika mkono wa kuume wa Mungu. Kuelewa jinsi alivyofanyika mwanadamu ni jambo la ajabu na miujiza ya Mungu, lakini kwa sababu Mungu alitupenda sisi, Yesu alikuja (Yohana 3:16).

"Yeye ni Mungu wetu aliye hai na anatujali sisi. Ameuweka ufalme wake duniani kama ule ulioko mbinguni. Ufalme huo ni kanisa."

**Ukweli Katika Maisha Yetu**

"Je, unawafahamu wale wanaopenda kumtii Mungu? Ni kanisa la Mungu. Je, umemwungama Yesu kama Mwokozi na Bwana? Kama ndivyo, wewe pia ni sehemu ya ufalme wa Mungu. Je, unafikiri Mungu anataka kanisa lake lifanye nini? Ni matendo yapi yanayomfurahisha Mungu? Ni mambo yapi yanayomchukiza Mungu? Soma 1 Yohana 1:9. Tufanye nini tunaposhindwa kumpendeza Mungu? Kama tukiomba msamaha na tukiwa tayari kumpendeza katika mioyo yetu, basi tutakuwa kanisa la kweli la Mungu."

**Kuomba**

1. Omba kuwa Mungu atakupa hekima ya kulifundisha somo hili.
2. Mwombee mwanafunzi ye yote yule ambaye bado hajawa mshiriki wa kanisa la Bwana.

SURA YA TATU

# KUWA SHAHIDI

## KUJITAYARISHA KUFUNDISHA

Somo Kutoka: Marko 16:15-18

Vifungu vya Leo: Mathayo 28:16-20; Luka 24:44-49; Matendo 1:1-8

**Kifungu cha Kukumbuka**

> "Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu" (Mathayo 28:19).

Kusudi la Somo Hili: Kuwafundisha wanafunzi kuwa kazi ya kanisa ni kuwaeleza wengine juu ya Kristo na yale aliyofanya.

Vitu vya Kusaidia Kufundisha: Karatasi pamoja na kalamu kwa kila mwanafunzi.

**Msingi wa Somo Hili**

Vitabu hivi vitatu vya maandiko vemeeleza maneno ya mwisho ya Kristo kabla ya kupaa mbinguni. Haya ni maneno muhimu sana kwetu.

Katika Mathayo 28:19-20, Kristo anaonyesha kazi ya shahidi. Maneno "Basi, enendeni" mara nyingi tafsiri yake ni mnavyokwenda au "wakati mkienda." Kuwafanya wanafunzi ni kitu cha kawaida kwa Mkristo kufanya wakati ule ule akiendelea na shughuli zake za kila siku. Mkristo wa kweli anaposafiri kutoka sehemu moja kwenda nyingine, atapenda kuwaeleza wengine habari za Kristo.

Lengo la kuwa mshahidi ni kuwafanya wanafunzi. Mwanafunzi ni yule anayeiamini injili na anaendelea kujitahidi kuwa kama Kristo. Mwanafunzi wa kweli hujibidisha kuwafanya wanafunzi wengine kwa kuwatolea ushahidi. Huwaleta wengine kwa Kristo ili wazae matunda.

Matokeo ya kazi ya ushahidi katika kumfanya mwanafunzi ni pamoja na ubatizo. Ubatizo ufuate imani katika Kristo. Ubatizo hauwezi kumwokoa mtu ye yote. Kristo pekee ndiye awezaye kutuokoa. Ubatizo ni ishara kwa wengine kuwa tumeyaweka matumaini yetu katika Kristo.

Katika Luka 24:44-49 tunapata habari zaidi za ushahidi. Ujumbe wa ushahidi upo katika vifungu hivyo vitatu. Kifungu cha 44 kinamtaja Kristo kama aliyekamilisha unabii wa maandiko. Yeye ni Masihi. Kristo aliwaeleza wanafunzi wake kuhusu unabii katika kifungu cha 46. Aliwakumbusha kuwa aliteswa akafa na akapaa tena kutokana na unabii huo.

Zaidi Kristo aliahidi nguvu za Roho Mtakatifu kwa wanafunzi wake. Roho Mtakatifu huleta nguvu kwa yule anayetoa ushahidi ili wale wanaozipokea habari hizo waweze kuamini. Neno ushahidi kama lilivyotumiwa katika Luka 24:48 na Matendo 1:8 linatuonyesha kuwa kazi yetu ni kuwa shahidi.

Matendo 1:8 inatupa ujumbe wenye nguvu zaidi kuliko maandiko mengine. Kristo anatuamuru tuwe mashahidi. Shahidi huenda kila mahali akiwa na ujumbe maalum kuwa Yesu anaokoa wote wanaomwamini.

## KULIFUNDISHA SOMO HILI

**Utangulizi**

Sema: "Tuseme leo asubuhi ulipokuwa njiani ukija kanisani uliiona ajali ya basi. Labda askari atakutaka ufike mahakamani ili utoe ushahidi. Je, kama shahidi utafanya

nini?" (Wape nafasi wengi wapate kujibu.) "Shahidi anaeleza kwa ufasaha yale aliyoyaona na anayoyajua.

"Wakristo pia huitwa mashahidi. Je, unafikiri hiyo ina maana gani?" (Shahidi wa Kristo ni yule anayeeleza yale anayoelewa kuhusu Kristo.)

Sema: "Katika Luka 24:44-48, Yesu anawaambia wanafunzi wake baada ya kufufuka kwake kuwa aliteswa, akafa, akafufuka tena na kuwa nao ni mashahidi. Aliwaamuru wayaeleze yote yale waliyoyaona. Kwa hivyo wanafunzi wakawa mashahidi wa yale yote Kristo aliyokuwa amefanya."

Uliza: "Je, sisi wenyewe ni mashahidi wa nini katika maisha yetu ya Kikristo?" Majibu yaweza kuwa: Yesu anaishi ndani yetu; Yesu ananisaidia kushinda matatizo, Yesu husamehe dhambi na huleta amani au Yesu huleta furaha katika maisha yetu.

Sasa waulize wanafunzi wako waeleze jinsi Yesu alivyowasaidia. Taarifa hizo tunaziita ushuhuda. Mtu anayetoa ushuhuda anaitwa shahidi.

Sema: "Ebu tuseme kuwa uliitwa kama shahidi kutoa ushuhuda wa yale uliyoyaona kwenye ajali ya basi. Ingekuwaje, kama ungeanza kwa kusema, 'Sikumbuki cho chote.' Je, ungekuwa shahidi mzuri au hapana? Shahidi mzuri lazima afahamu ni nini kilichotokea ili aweze kukieleza ili wote wanaosikia waweze kuelewa."

**Maelezo**

Sema: "Katika Luka 24:44-46, Yesu anawakumbusha wanafunzi wake juu ya yale yote waliyoyaona na kusikia kumhusu yeye. Tukikumbuka yale yote Kristo alivyotufanyia katika maisha yetu, inaukamilisha ushahidi au ushuhuda wetu.

"Shahidi mzuri wa ajali anapaswa kukumbuka yale yote aliyoyaona na anayoyajua. Kwa njia hiyo hiyo Mkristo anapaswa kukumbuka alivyompokea Kristo na alivyokuwa Mkristo. Anapaswa kuwaeleza wengine katika njia ambayo wataelewa.

"Katika Matendo 1:7-8 tunakumbushwa kuwa sisi kama mashahidi ni lazima tuwajibike. Yesu anatufundisha kuwa tusiwe na hofu kuhusu kule mbinguni. Mwisho wa nyakati utakuja siku moja, lakini sasa tunapaswa kuwajibika kama mashahidi wake.

"Kazi ya kanisa ni kutoa ushahidi kuhusu nguvu za Mungu kwa njia ya Yesu Kristo. Washiriki wa kanisa lazima waieleze dunia yale yote Kristo aliyofanya."

**.Ukweli Katika Maisha Yetu**

Uliza: "Je, unamfahamu mmoja ambaye ni shahidi mzuri? Je, unaweza kumkumbuka yule aliyekueleza habari za Yesu?"

Mpe kila mwanafunzi karatasi pamoja na kalamu. Waambie waandike taarifa fupi jinsi walivyomfahamu Yesu. Baada ya kumaliza, uliza baadhi yao wasome majibu yao.

Sasa waulize, "Je, Kristo amefanya jambo lo lote kwako tangu uwe Mkristo?" Waorodheshe baadhi ya mambo. Waandike wazi na kwa ufasaha katika majibu yao. Waulize baadhi yao kusoma yale waliyoandika.

Sasa uliza: "Je, Kristo amekutendea lo lote katika maisha yako juma hili?" Waambie waorodheshe majibu yao na wasome yale waliyoandika.

Shahidi mzuri anapaswa kueleza jinsi alivyompokea Kristo na jinsi anavyofanya kazi nao katika maisha yao kila siku. Ushuhuda lazima uonyeshe yale Kristo aliyowatendea karibuni, na jinsi wao wenyewe walivyopata Ukristo.

**Kuomba**

1. Omba kuwa wanafunzi wako watakuwa mashahidi wazuri.

2. Omba kuwa wale walio Wakristo watampokea Yesu kama Mwokozi wao.

SURA YA NNE

# KANISA HAPO MWANZO

## KUJITAYARISHA KUFUNDISHA

Somo Kutoka: Matendo 5:1-6:5

Vifungu vya Leo: Matendo 4:32-37

**Kifungu cha Kukumbuka**

> "Petro na mitume wakajibu, wakisema, Imetupasa kumtii Mungu kuliko wanadamu" (Matendo 5:29).

Kusudi la Somo Hili: Kuwafundisha wanafunzi wangu kuwa kanisa sio tu linahubiri injili ya Kristo, bali huyatimiza pia mahitaji ya washiriki.

Vitu vya Kusaidia Kufundisha: Karatasi pamoja na kalamu kwa kila mwanafunzi.

**Msingi wa Somo Hili**

Kanisa lilianza baada ya kufufuka kwa Yesu. Wale watu ambao walikuwa na imani, katika Kristo na wakawa kanisa lake walijiunga pamoja kwa kuhubiri na kufundisha. Kwa kawaida makutano yaliendeshwa na mtume kama akiwepo. Hawakutumia vitabu vingine vya nyimbo zaidi ya Zaburi katika Biblia. Kila mara mitume walihubiri injili sokoni, na watu wengi wakaliamini neno kwa uwezo wa nguvu za Roho Mtakatifu.

Makuhani na viongozi waliwachukia mitume kwa sababu watu wengi walikuwa wanamwamini Yesu. Mahubiri ya mitume yaliwashambulia viongozi hawa wa dini kama wauaji wa Yesu. Viongozi hawa wa dini ambao waliitwa Mafarisayo na Masadukayo walitumia kufahamika kwao kisiasa kuwaua, kuwatesa na kuwatendea vibaya Wakristo kwa sababu waliogopa mafundisho yao na kufahamika kwao.

Wanafunzi waliendelea kuhubiri na kuponya kwa jina la Yesu. Matokeo yake ni kuwa Wakristo walizidi kutendewa vibaya. Wakristo wengi walipoteza kazi zao na biashara zao ziliharibika. Kwanza Wakristo wengi walikuwa maskini. Roho Mtakatifu aliwaongoza wautumie upendo wa Kristo na kushiriki vile walivyokuwa navyo na wengine. Kushiriki vitu vyote kwa pamoja ni lengo la baadhi ya serikali duniani leo, lakini bila upendo mkuu wa Kristo kuibadilisha mioyo ili ipende kushiriki mahitaji, serikali hizi zimeshindwa.

Matendo 4:34 inasema, "Wala hapakuwa na mtu mmoja miongoni mwao mwenye mahitaji..." Baraka za Mungu kwa watu wake, hutosheleza mahitaji ya kila mmoja. Mungu alitoa mahitaji ya kutosha kwa kanisa lote. Hakuna aliyekuwa na mahitaji. Hata wale waliotoa vile walivyokuwa navyo waliona mahitaji yao yanatoshelezwa pia.

Vifungu vya 34-37 vinatuambia maana halisi ya mtu kujikana mwenyewe na kuuchukua msalaba wake. Hawa Wakristo wa mwanzo walimwamini Mungu kuwa atawatimizia mahitaji yao kwa hivyo walitoa vyote walivyokuwa navyo ili wamfuate Bwana.

Sio kila mmoja aliyeuza nyumba au kiwanja chake kwa sababu Wakristo hawangepata mahali pa makutano kama wasingefanya hivyo. Kuacha kazi hakukutajwa katika vifungu hivi. Kila mmoja lazima aendelee kuihudumia jamaa yake na wakati huo huo kuwasaidia wenye mahitaji. Kristo alijitoa kabisa mwenyewe kwa ajili ya wengine, lakini pia alifurahi alipomtembelea Lazaro nyumbani mwake.

Tukifuata kifungu hiki cha maandiko kuna habari za kwanza za wanafiki. Anania na Safira walijionyesha wametoa vyote walivyokuwa navyo kwa Mungu. Walitaka waonekane wazuri mbele za wengine, lakini walikuwa hawajamruhusu Bwana aibadilishe mioyo yao. Mungu hudharau moyo wenye

uovu unaojifanya kuwa wa kimungu. Anania na Safira walikufa kwa sababu ya matendo yao. Itakuwa vivyo hivyo kwa yule atakayejifanya kuwa mzuri. Watakufa kiroho. Moyo wa kweli wa kutoa na kumjali jirani yako hutoka kwa Roho Mtakatifu.

## KULIFUNDISHA SOMO HILI

### Utangulizi

Uliza: "Je, mahitaji ulio nayo ni yapi?" (Yanaweza yakawa chakula, nguo, ada ya shule, nyumba na mengineyo.) Nani anakupa mahitaji haya? (wazazi, ndugu)

Sema: "Familia hutunzana. Wazazi hutunza watoto, na baadaye wazazi wanapozeeka, watoto huwatunza wazazi wao. Kanisa pia ni familia. Kanisa ni familia ya Mungu.

"Kwa nini unafikiri mahitaji mengine ya washiriki wa kanisa lako hayatoshelezwi?" (Watu wengine hawazifahamu habari zao, watu wengine ni wachoyo, watu wengine hawawajali.) "Kristo alituamuru tupendane sisi kwa sisi ili dunia ielewe kuwa sisi ni wanafunzi wake.

"Kijiji kinalionaje kanisa ambalo haliangalii watu ambao wana shida na wanasikia baridi kwa sababu hawana nguo au makaa? Je, tunaonyesha upendo wa Yesu duniani?

"Je, kanisa lako lingewasaidiaje wenye mahitaji katika kijiji chako?" (fedha, chakula, nguo)

"Kutoa pasipo na uchoyo ili wengine waweze kulishwa na kuvalishwa ni ushuhuda mkubwa wa upendo wetu na imani katika Kristo. Tunapaswa kuacha vile vitu vya ziada tunavyotumia (kama peremende, soda) ili tuweze kuwa na ziada kuwapa wale wenye mahitaji. Labda darasa letu litaanza kukusanya fedha za kumsaidia yule ambaye hana ada ya shule au nguo za shule".

**Maelezo**

"Kanisa halihubiri tu habari za Yesu, pia hutoa kwa wengine kama Kristo alivyotuonyesha. Anampenda kila mmoja awe ni maskini, mgonjwa au aliyelemewa.

"Kristo hakuwavumilia wale matajiri waliokuwa wakiwadanganya maskini na kujiwekea faida wao wenyewe. Alisema kuwa ni rahisi ngamia kuingia kwenye tundu la sindano kuliko kwa tajiri kwenda mbinguni. (Mathayo 19:16-24)

"Baadhi ya matajiri hawapendi kushiriki mali zao na wengine, ha hawamtolei Mungu utukufu kwa vile walivyonavyo. Wanajivunia mali zao hata kama wamemdanganya maskini kuzipata."

Sasa ebu tuwatazame Lazaro, Maria na Martha. Walikuwa na mali. Walikuwa na nyumba ambayo walimfungulia Yesu na wanafunzi wake. Walijitoa kwa kazi ya kanisa. Walitayarisha chakula na kuonyesha ukarimu kwa wale wote Yesu aliokuja nao. Lazaro alipokufa, walikuwa na marafiki wengi walioshiriki nao huzuni yao. Walimwogopa Mungu na kumwabudu.

Mtu mmoja alisema kuwa mtu mwenye mali ana raha, lakini ana huzuni kama mali yake inamtawala. Watu wengi wana mizigo ya mali zao. Ni lazima wajitahidi kuilinda wezi wasiibe. Wengine wanayo furaha kwa sababu wamejifunza kushiriki mali zao kwani vitu vyote vizuri vyatoka kwa Bwana.

**Ukweli Katika Maisha Yetu**

Sema: "Kila mmoja wenu aandike orodha ya vitu alivyonavyo. Andika pamoja na fedha, nguo, vifaa vya shule, afya nzuri, mwili imara na vitu vingine. Sasa iangalie hiyo orodha yako kwa makini. Ni vitu vipi kati ya hivyo ni vya lazima? Je, ungeshirikije vile ulivyo navyo na watu wengine?"

Uwe na hakika umetaja fedha ya akiba. Wakumbushe kuwa fungu la kumi la fedha zao ni mali ya Mungu. Wakumbushe kuwa, waitumie miili yao iliyo imara, na nguvu (na muda) kuwasaidia wazazi wao na wale walio wazee.

**Kuomba**

1. Omba kuwa wanafunzi wako watajifunza kuwa wanavyo vitu vya kushiriki.

2. Omba kuwa kanisa lako litawajali zaidi wale wenye mahitaji.

SURA YA TANO

# KUONGOZWA NA ROHO

## KUJITAYARISHA KUFUNDISHA

Somo Kutoka: Wagalatia 5:22; Warumi 8:16

Vifungu vya Leo: Matendo 13:1-4; 16:6-10; Warumi 8:9-10, 14

**Kifungu cha Kukumbuka**

> "Kwa kuwa wote wanaoongozwa na Roho wa Mungu, hao ndio wana wa Mungu" (Warumi 8:14).

Kusudi la Somo Hili: Kuwafundisha wanafunzi wangu kazi ya Roho Mtakatifu katika kanisa. ika '

Vitu vya Kusaidia Kufundisha: Andika kichwa hicho ubaoni au kwenye karatasi kubwa.

**Mingi wa Somo Hili**

Katika somo la kwanza la kitabu hiki umejifunza kuwa Kristo ndiye kichwa cha kanisa. Yeye ndiye anayeliongoza kanisa kwa njia ya Roho Mtakatifu. Kila mara Mungu amewatumia walioongozwa na Roho kufanya mapenzi yake yajulikane kwa wafuasi wake. Utaratibu huu haujabadilika vizazi hadi vizazi. Bado Mungu anazungumza na wanadamu na makanisa kwa njia ya Roho Mtakatifu.

Katika Matendo 13:1-4, Roho Mtakatifu aliwaongoza viongozi wa kanisa kuwachagua Paulo na Barnaba kwa wito maalum. Paulo na Barnaba walifahamu kuwa Roho Mtakatifu alikuwa akiwaongoza waondoke Antiokia wakawe wamisheni. Roho Mtakatifu aliliongoza lile kanisa la mwanzo kwa kazi yake ya kwanza ya utumishi nje ya kanisa, utumishi wa kimisheni.

Vifungu vya 2 na 3 vinasisitiza jambo jingine muhimu kuhusu Roho Mtakatifu. Alisema na washiriki wa kanisa wakati wakiwa wanaabudu. Angalia kuwa manabii na waalimu walifunga; wakaomba na kumtumikia Bwana kabla ya kuongozwa na Roho Mtakatifu. Walikuwa wakimsifu Bwana na Roho Mtakatifu akasema nao.

Kifungu cha 3 kinaonyesha njia nyingine ambayo Roho Mtakatifu aliwaongoza watu hawa. Roho Mtakatifu aliwaongoza wawawekee mikono Paulo na Barnaba. Kuwawekea mikono ina maana kuwa walikubaliana na wito wa Paulo na Barnaba kufanya kazi ya umisheni na kuwa angewaongoza katika utumishi wao. Katika sehemu nyingi watu husalimiana na wale wanaowaita marafiki, wale ambao wangeshiriki chakula nao. Kwa njia hiyo hiyo, kuwekea mikono ina maana zaidi kama ile tuliyonayo ya kijamii ya kusalimiana kwa kushikana mikono. Hii iliwaonyesha Paulo na Barnaba upendo wa Kikristo na kusaidiana kwa njia ya maombi na fedha.

Paulo na Barnaba walitegemea Roho Mtakatifu awaongoze katika kazi yao ya umisheni. Angalia kifungu cha 4. Wale waliojazwa Roho Mtakatifu waliendelea kuongozwa na Roho Mtakatifu katika maisha yao ya kila siku na katika maamuzi muhimu.

Roho Mtakatifu aliwafungia milango Paulo na Barnaba pia. Mungu anao mpango mkubwa zaidi kuliko sisi wenyewe tunavyofahamu. Katika Matendo ya Mitume 16:6-7, Roho Mtakatifu aliwakataza wasilihubiri Neno katika Asia. Aliwapeleka Makedonia. Roho Mtakatifu haachi wito wa kuwaita watu kwa utumishi. Pia huchagua ni sehemu gani hao watu waende kuhudumu.

Roho Mtakatifu katika maisha ya mwamini ni ishara kwa wengine katika kanisa kuwa fulani ni Mkristo. Warumi 8:9-11

inaeleza kwa wazi kuwa yule aliye na Kristo anaye Roho wa Kristo katika maisha yake. Wakristo wa kweli wataendelea kuongozwa na Roho Mtakatifu. Hata hivyo Roho Mtakatifu hawezi kukaa mahali pale penye dhambi. Kwa hivyo yule Mkristo anayefanya dhambi, kama sote tufanyavyo, lazima atubu kila siku dhambi zake ili asafishwe naye Roho Mtakatifu aweze kumwongoza.

## KULIFUNDISHA SOMO HILI

### Utangulizi

Uliza: "Nani analiongoza kanisa?" (Kristo) "Katika somo letu la kwanza tulijifunza kuwa Kristo ni kichwa cha kanisa. Kristo analiongoza kanisa kwa njia ya Roho Mtakatifu."

Uliza: "Je, umeshajisikia kuwa Bwana anazungumza nawe juu ya jambo fulani? Bwana huzungumza nasi kwa njia ya Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu hatatuongoza kufanya kinyume cha Biblia au matakwa ya Mungu.

"Kama hujajisikia kuwa Mungu anazungumza nawe, basi labda hujamwomba Bwana akuongoze. Huwaongoza wale tu wanaopenda uongozi wake. Kizuizi kingine ni dhambi ambayo haikuungamwa. Wakristo wote humkosea Bwana na hutenda dhambi, lakini yule anayeshindwa kuungama na kutubu huzuia kazi ya Roho Mtakatifu katika maisha yake.

"Ebu tuangalie ni kwa njia zipi Roho Mtakatifu aliwaongoza Wakristo katika lile kanisa la mwanzo." Mwanafunzi asome Maandiko. Mnaposoma pamoja, waambie wanafunzi yale mliyojifunza katika Msingi wa Somo Hili na katika Maelezo.

### Maelezo

Roho Mtakatifu aliwaongoza wale Wakristo wa mwanzo katika kazi ya utumishi. Roho yule yule anatenda kazi hata leo.

Roho Mtakatifu aliyemwita Paulo na Barnaba kwa kazi ya umisheni anawaita watu kutoka katika kanisa lako. Huwaita wachungaji, waalimu wa Shule ya Jumapili, mashemasi na wengine kufanya kazi ya kanisa. Wale wanaofanya kazi katika sehemu hizi lazima waitwe na Roho na kuongozwa na Roho.

Mara nyingine hata hivyo, baadhi ya wale walioitwa na Bwana, hawajibu. Wale wanaoitikia wito hushindwa kuendelea katika Roho na kuiruhusu dhambi kuzuia nguvu zao katika Roho. Wakristo hawa hawazai matunda. Hawapati kuelewa hasa amani ya kweli, furaha, uvumilivu na matunda mengine ya kiroho yaliyoorodheshwa katika Wagalatia 5:22.

Roho humwongoza Mkristo kujua sehemu asizohitajika kuwepo. Kuna kazi nyingi za kufanya katika kanisa na siyo mtu mmoja tu ameitwa kufanya kazi hizo zote. Kuna karama nyingi za kiroho na aina nyingi za utumishi. Kila mshiriki wa kanisa lazima atimize wajibu wake na kujikana kwa mambo mengine (Matendo 16:6-10).

**Ukweli Katika Maisha Yetu**

Sema: "Roho Mtakatifu humwongoza kila mwamini anayemruhusu ayatawale maisha yake. Fikiria wakati ambao ulijisikia kuwa Mungu anakuongoza katika njia maalum." Wape muda wa kutafakari. "Ni wakati gani uliopita ulipojisikia kuwa kuna anayeongoza maisha yako?" (Usihitaji majibu.) "Kama ni wakati mrefu uliopita, je, dhambi imekuingia na kukuzuia usiongozwe na Roho."

Wanafunzi waombe kimya kimya wakimwomba Roho Mtakatifuf awaongoze. Waambie waungame kwa Bwana dhambi zo zote zile walizo nazo na waombe kusamehewa dhambi hizo.

Wakumbushe kuwa wanapawa kufanya hivyo kila mara na waweke kumbukumbu katika karatasi juu ya yale ambayo

Roho Mtakatifu amewaongoza kufanya. Roho Mtakatifu kila mara husema nasi kwa njia ya maandiko. Labda atawaongoza kuyasoma maandiko na kutumia muda zaidi katika maombi. Waambie wanafunzi kuwa juma lijalo utahitaji kumbukumbu zao.

**Kuomba**

1. Mwombe Mungu akuongoze kwa Roho wake, wakati ukilifundisha somo hili.

2. Mwombe afanye kazi katika maisha ya wanafunzi wako juma hili.

SURA YA SITA

# TU MMOJA INGAWA WENGI

## KUJITAYARISHA KUFUNDISHA

Somo Kutoka: 1 Wakorintho 13; Wafilipi 3:4-8

Vifungu vya Leo: Warumi 12:3-18

**Kifungu cha Kukumbuka**

> "Kwa kuwa kama vile katika mwili mmoja tuna viungo vingi, wala viungo vyote havitendi kazi moja; vivyo hivyo na sisi tulio wengi tu mwili mmoja katika Kristo, na viungo, kila mmoja kwa mwenzake" (Warumi 12:4-5).

Kusudi la Somo Hili: Ili niwafundishe wanafunzi wangu kuwa kila mshiriki katika kanisa anao wajibu na hakuna aliye bora kuliko mwingine.

Vitu vya Kusaidia Kufundisha: Ubao au karatasi kubwa. Andika kichwa cha habari hii ubaoni.

**Msingi wa Somo Hili**

Paulo aliwaandikia barua Warumi ili kulisaidia kanisa lielewe maisha ya Kikristo. Paulo hakuwa ameyatembelea hayo makanisa ya Roma. Kama yalivyo makanisa mengi, kanisa lile la Roma lilipingana na tofauti za watu, tofauti za kabila, na tofauti za elimu. Wayahudi walikuwa na historia ndefu ya chuki na kutowaamini Watu wa Mataifa. Kanisa lile la mwanzo lilifundisha kuwa wote walikuwa Wakristo na walikuwa sawa mbele za macho yake.

Katika barua nyingine Paulo alijihusisha na swali la mwenendo mbaya. Katika Wakorintho wa Kwanza 13 ni kinyume kabisa cha mwenendo huo. Katika Wafilipi 3:4-8, Paulo anawakumbusha Wafilipi juu ya yale yote aliyoyapata

yeye na kusema hayo yote yalikuwa ni kama mavi mbele za Bwana. Mtu pekee hawezi kufanikiwa kama yale anayoyatenda ni kinyume cha mpango wa Mungu na utukufu wake.

Wayahudi kila mara waliwasema watu wa mataifa kwa sababu hawakutahiriwa. Watu wa Mataifa kila mara waliwashitaki Wayahudi kwa kutowatendea vizuri. Tofauti kati ya Wayahudi na Watu wa Mataifa zilikuwa za rangi, mila na za kidini. Historia ya Wayahudi ni yenye msingi wa sheria kali za kidini na kumcha Mungu. Watu wa Mataifa msingi wao umetokana na upagani na miungu mingi. Makundi haya mawili yaliyo tofauti walifanywa mwili mmoja katika Kristo. Lakini matatizo bado yalikuwepo kwa Wayahudi ambao walipokea au kuwatenga watu kwa misingi ya sheria za dini yao ya zamani. Vivyo hivyo nao watu wa mataifa walikuwa na matatizo mengi kama kutoa kafara za nyama kwa sanamu na kama hizo nyama wangekula au la. Pia, kwa Wayahudi wao wenyewe, walijiona kama watu duni.

Paulo alisema kuwa kila mmoja ajiangalie jinsi anavyojifikiria yeye mwenyewe. Alishauri pawepo na uamuzi wenye maana kama Mungu alivyotuonyesha sisi ambao tu katika Kristo. Hatuna mshiriki wa kanisa aliye bora kuliko mwingine. Mchungaji, mwalimu, kijana wa kwaya, mtoto mdogo na watu wazee wote tu sawa mbele za Mungu. Mungu anampenda kila mmoja.

Mungu alilipenda kanisa kwa hivyo alitoa vipawa kwa wafuasi wake. Vipawa hivi vinatofautiana na kila kimoja kina wajibu tofauti na kingine. Kila kimoja kinaheshimika mbele za Mungu. Msingi wa uwelewano katika kanisa ni kulielewa wazo hili. Kila mmoja ni muhimu, na kila jambo ni muhimu. Kila mshiriki lazima atumie kipawa chake kwa uwezo wake wote. Hakuna hata mmoja aliye na haki au uwezo wa kumhukumu mwingine, au umashuhuri wake au thamani yake mbele za Mungu.

Katika Warumi 12:10, Paulo anasisitiza uhusiano wa kweli kati ya washiriki wote. "Kwa pendo la udugu, mpendane ninyi kwa ninyi; kwa heshima..." Hakuna mtu mzima aliye bora kuliko kijana; vivyo hivyo hakuna kijana aliye bora kuliko mwingine. Hakuna taifa, hakuna kabila lililo bora kuliko jingine.

Katika kifungu cha 13 kinaeleza hata zaidi kuhusu amri za Mungu. Anasema ni lazima tujitahidi kutimiza mahitaji ya wengine na kuwa wakarimu. Jambo muhimu ni kuwatumikia wengine na sio kuwahukumu.

Maneno makali sana ya Paulo yapo katika vifungu vya 17 na 18. Mkristo halipi uovu kwa uovu, lakini tuangalie yaliyo mema machoni pa watu wote. Hii ni zaidi yatuwezavyo kutenda kwa uwezo wetu. Lakini ili Mkristo awe na mwenendo huo, Kristo lazima awe mtawala wa maisha yake.

## KULIFUNDISHA SOMO HILI

### Utangulizi

Uliza: "Je, unaweza kumfikiria ye yote yule shuleni kwako au nyumbani ambaye kila mtu humtusi au kumdanganya? Je, mtu huyu ni kati ya wale wanaofikiriwa na watu ni wa hali ya chini au asiye na uwezo? Kwa nini unafikiri watu hupenda waonekane bora kuliko wengine? Watu kila mahali hufurahia kuwa bora kuliko wengine. Mwenendo huu wa majivuno ni wa dunia sio wa Mungu.

"Paulo alisema kuwa Wakristo lazima wapendane kwa heshima na sio wajione wao ni bora zaidi kuliko wanavyostahili. Biblia inafundisha tofauti hizi za mwenendo - mwenendo wa upendo."

### Maelezo

Watu hata leo ni sawa na watu siku zile za Paulo. Wanataka wawe bora. Wanataka wawe bora kuliko watu wengine. Watu

hutumia visingizio vingi kufikia lengo lao. Paulo alisema kuwa katika Kristo hakuna tofauti kati ya Myahudi na Mgiriki. Wengine wanasema kuwa wanaume wana akili zaidi kuliko wanawake. Paulo alisema kuwa katika Kristo hakuna mwanaume wala mwanamke. Mawazo ya kuwa bora ni ya Shetani. Wazo kuwa Mungu alituumba sote sawa linahitaji upendo, amani na umoja.

Kanisa leo linapata shida hizo hizo. Wengine hujiona kuwa kwa sababu wana fedha au shahada ya chuo kikuu, basi wao ni viongozi bora. Mungu anasema kuwa atawainua wanyenyekevu na kuwakataa wenye majivuno. Mapenzi ya Mungu ni kuwa viongozi watamtumaini yeye na siyo kujitumaini wao wenyewe.

**Ukweli Katika Maisha Yetu**

Uliza: "Je, unamfahamu mtu ye yote ambaye alijionyesha kuwa bora kuliko wewe? Je, walikufanya ujisikieje? Sababu ya majivuno yao ilikuwa nini?" (fedha, uzuri, akili) "Je, mambo haya ni mazuri katika kuwahukumu watu?

"Labda umeshajaribu kuwa bora kuliko mtu mwingine. Labda katika mstari fulani wa watu wewe uliwapita tu na kuwa wa kwanza mbele. Hii ina maana kuwa wewe ulijiona bora zaidi kuliko hao wengine waliokuwa wakingoja.

"Juma hili angalia ili uwatendee sawa watu wote. Salimu wanafunzi wote wa darasa lako, na siyo rafiki zako tu. Mtendee kila mmoja unayekutana naye kuwa sawa nawe.

**Kuomba**

1. Muombe Mungu ili akuonyeshe njia kwani unashindwa kuwatendea wengine sawa na uombe msamaha wa dhambi hiyo.

2. Omba ili upewe njia za kuwaonyesha wanafunzi wako umuhimu wa mwenendo wao. Pia, wakati wo wote wa somo hili wape nafasi wanafunzi ili waweze kutoa ushahidi jinsi Roho Mtakatifu alivyowaongoza juma hili. Juma lililopita uliwaambia kuwa utahitaji hizi kumbukumbu zao.

SURA YA SABA

# TUMECHAGULIWA KWA NJIA YA KRISTO

## KUJITAYARISHA KUFUNDISHA

Somo Kutoka: 2 Wakorintho 5:17-19

Vifungu vya Leo: Waefeso 1:1-4

**Kifungu cha Kukumbuka**

> "Kwa kuwa alitangulia kutuchagua, ili tufanywe wanawe kwa njia ya Yesu Kristo, sawasawa na uradhi wa mapenzi yake" (Waefeso 1:5).

Kusudi la Somo Hili: Kuwafundisha wanafunzi wangu ina maana gani kuwa katika Kristo.

Vitu vya Kusaidia Kufundisha: Ubao au karatasi kubwa.

**Msingi wa Somo Hili**

Katika barua hii kwa Waefeso, Paulo anaeleza mpango wa Mungu katika kulianzisha na kulikamilisha kanisa. Paulo ametumia maneno ya aina mbalimbali kufundisha juu ya wokovu katika Kristo. Baadhi ya maneno hayo yake ni: katika yeye, kwa njia yake, katika upendo na katika Kristo.

Matumizi na maana ya maneno haya inatusaidia tuelewe maana ya "kutuchagua" katika kifungu cha 5. Vikundi vingine vya Wakristo vinaamini kuwa maana yake ni kuwa Mungu anawaita wale tu wanaoitikia upendo wake. Wengine wanaamini kuwa wako huru kufanya lo lote waliloamua kwa sababu Mungu alikwisha tuchagua au kuamua kabla.

Kwa sababu Paulo alitumia maneno katika yeye au katika Kristo, tunaweza kuelewa maana halisi ya neno "kutuchagua."

Kwanza kabisa kuchagua ina maana ya kupanga kabla. Kwa hali hii, amepanga kitu fulani kwa ajili yetu. Mungu amepanga nini? Mungu alipanga kuwa tutaalikwa kuwa watoto wake kwa njia ya Kristo. Tunapomkubali Kristo kama Mwokozi, tunaalikwa katika jamii ya Mungu.

Mungu pia alitupangia tuwe wasio na hatia na tuwe watakatifu. Je, wenye dhambi watakuwaje wasio na hatia tena walio watakatifu? Ni kwa njia ya Kristo tu haya yanaweza kutendeka. Katika yeye tunafanywa watakatifu na wasio na hatia, siyo kwa ajili ya haki yetu sisi wenyewe, lakini kwa njia ya haki ya Kristo.

Mungu alipanga mambo haya yote yatokee katika uhai wetu tukiwa "katika Kristo." Kifungu hiki hakisemi Mungu alimchagua nani au nani hatakuwa katika Kristo. Badala yake alipanga kuwa wale wanaomkubali mwanawe watafanywa kama wana na pia watakuwa wasio na hatia na watakatifu.

Tunapomkubali Kristo, tunakuwa "katika Kristo." Kwa ajili hiyo, tumebarikiwa kwa kila baraka ya kiroho, kama upendo, furaha, amani na nyingine nyingi. Tunakuwa watakatifu na wasio na hatia kama wanavyofanywa watoto wake. Tunapata neema yake, ukombozi na msamaha wa dhambi. Mungu ametupa sisi kufahamu maajabu ya mapenzi yake, na ametupa urithi, yaani uzima wa milele.

Mwishowe, tumepigwa muhuri wa Roho Mtakatifu. Muhuri ni ushahidi kuwa kitu fulani ni amri. Sheria zinazotumika serikalini na amri zinao muhuri wa serikali. Kwa kuwa Roho Mtakatifu ni muhuri wa Mungu, sisi tulio naye Roho Mtakatifu tuna imani kuwa tutapata uzima wa milele Yesu atakaporudi.

Tumeokolewa katika Kristo kwa kusudi maalum, kwa ajili ya kusifu utukufu wake. Maneno haya yanatangaza lengo letu: kuishi maisha ambayo wengine wataona jinsi Mungu alivyo

mkuu. Maana moja ya neno, utukufu, ni kutoa mawazo yaliyo sahihi juu ya Mungu. Kama tutaishi maisha ya uovu, basi watu wataona kuwa Mungu hayupo au kuwa Mungu ni mwovu. Kama tutaishi maisha yasiyo na hatia, maisha mazuri, watu watajua kuwa Mungu yu mwema.

## KULIFUNDISHA SOMO HILI

**Utangulizi**

Uliza: "Je, unafikiri nini maana ya maneno 'katika Kristo'?" Wape muda kujibu maswali. Shiriki yale mliyojifunza kutoka kwa Msingi wa Somo Hili.

Sema: "Katika Kristo ina maana maisha mapya tulionayo katika yeye." Mwambie mwanafunzi aandike ubaoni au kwenye karatasi mambo yale yaliyo katika Kristo. Wengine wamsaidie. Baadhi ya majibu yaweza kuwa: kubarikiwa na baraka, kufanywa wana wa Mungu. Vitu vyote hivi vinakuwa mali yetu wakati tukimpokea Kristo.

Uliza: "Je, 'kutukuza utukufu wake' ina maana gani? Hili ndilo lengo jipya baada ya Kristo kuingia katika maisha ya mtu."

Waulize wanafunzi watoe maana ya neno, utukufu. Waambie yale uliyojifunza katika somo hili kuhusu utukufu.

**Maelezo**

Jadilianeni kwa makini mawazo yaliyopo juu ya neno "Katika Kristo". Je, umewahi kumwona mtu ye yote amevaa koti la kazi au vazi la kuzilinda nguo wakati wa kufanya kazi? Nguo zake za binafsi zimefunikwa na vazi hilo la kazi.

Tunapompokea Kristo kitu cha aina hiyo hutokea. Tunakuwa "katika Kristo." Mungu anapotuangalia

anamwona Kristo tu. Hatuoni sisi na dhambi zetu. Anauona ukamilifu wa Kristo ukiwa umetufunika.

Mkristo anapaswa kujikana mwenyewe na kubaki "katika Kristo" akiwa na hakika kuwa hamwoni mwingine. Wamwona mwingine. Wamwona Kristo kama kweli alivyo, mtakatifu na asiye na hatia, asiye laumiwa. Shetani anajaribu kuwashawishi Wakristo kuwa wao ni wazuri na kuwa hawahitaji kuwa kama Kristo. Anawashawishi watu wafurahie dhambi na kutafuta visingizio kwa makosa yao. Wakristo lazima wawe macho na uongo wa Shetani.

**Ukweli Katika Maisha Yetu**

Uliza: "Je, umeshajisikia kuwa Mungu yuko mbali nawe na wala hakujali? Somo la leo linatuambia kuwa Mungu anatupenda sisi sana hivyo kuwa anapenda kutufanya wana wake.

"Je, umeshajisikia kuwa hujui kama utakwenda mbinguni? Vifungu hivi vinatuambia kuwa tunao urithi sawa na Kristo aliyefufuka kutoka kwa wafu kwenda katika uzima wa milele. Roho Mtakatifu kama muhuri ni shahidi wa ukweli huo.

"Je, umeshafanya kitu cho chote ambacho kimemsifu Mungu? Je, umeshafanya cho chote ambacho kimemletea Mungu aibu? Kuna msamaha kwa wale wote ambao watatubu dhambi zao."

Fungu kwa sala ya kushukuru kwa kufanywa wana na sala ya toba kwa kushindwa kumtolea Mungu utukufu.

**Kuomba**

1. Omba kuwa Mungu atakusaidia kutenda yale yatakayomletea Mungu utukufu.

2. Omba kuwa utakuwa na imani na kuelewa kuwa urithi wako ni uzima wa milele.

SURA YA NANE

# KRISTO NI KICHWA CHA KANISA

## KUJITAYARISHA KUFUNDISHA

Somo Kutoka: Waefeso 1:1-23

Vifungu vya Leo: Waefeso 1:15-23

**Kifungu cha Kukumbuka**

> "Naye ndiye kichwa cha mwili, yaani, cha kanisa; naye ni mwanzo, ni mzaliwa wa kwanza katika wafu, ili kwamba awe mtangulizi katika yote (Wakolosai 1:18).

Kusudi la Somo Hili: Kuwafundisha wanafunzi wangu kuwa Wakristo ni sehemu ya mwili wa Kristo ambaye ni kichwa.

Vitu vya Kusaidia Kufundisha: Andika kichwa hicho ubaoni au kwenye karatasi kubwa.

**Msingi wa Somo Hili**

Katika sura ya saba tulijifunza neno "kutuchagua" likiwa na maana kuwa, Mungu aliwachagua waamini wote kuwa kama Kristo. Kwa waamini wote kuwa kama Kristo ndiyo lengo la barua kwa Waefeso.

Paulo anaianza sehemu hii kwa kusema kuwa alifahamu juu ya imani yao na hasa upendo wao kwa waamini wenzao. Naye aliendelea kuwaombea kukua kwao katika Kristo. Kukua na kukomaa alikosisitiza Paulo kunamtegemea Mungu ambaye ni mtoaji wa hekima. Mungu ndiye anayejitambulisha mwenyewe kwa waamini.

Paulo aliomba ili Waefeso waelewe kwa nini waliokolewa. Alitaka waelewe kusudi la Mungu la kuwaita kumletea Mungu utukufu. Tena zaidi ya hayo, Waefeso walihitaji kuelewa utukufu wa urithi wao, yaani uzima wa milele. Kristo ni wa mwanzo kufufuliwa katika uzima wa milele baada ya kifo, lakini sasa wale wote waliaminio jina lake pia watapata uhai huo.

Mwishoni Paulo anawakumbusha Waefeso kuhusu nguvu za Bwana. Nguvu za Mungu, zilimfufua Kristo kutoka kwa wafu. Nguvu zile zile zipo hata leo kwa kubadilisha maisha. Mungu wetu ni Mungu mwenye nguvu. Tena Paulo anabadilisha msisitizo wake kuwa; zawadi ya mwamini katika Kristo ni zawadi ile Kristo aliyonayo kwa njia ya dhabihu na ufufuo. Kwa ajili ya dhabihu hiyo ya haki, Mungu alimfufua kutoka kwa wafu na kumweka mkono wa kuume. Mtu anayekaa mkono wa kuume wa mfalme ni mtu anayeheshimiwa na mwenye mamlaka makubwa. Yesu yu pamoja na Mungu.

Yesu yu juu ya mamlaka yote, nguvu, utawala, juu ya kila jina litajwalo. Yeye ni wa kipeo cha juu, na mwenye mwenendo wa tofauti na mwingine. Yeye amekamilika. Anazitawala falme zote duniani na anazo nguvu kushinda nguvu zote za giza.

Paulo pia anasisitiza kuwa Kristo ni kichwa cha kanisa. Kanisa ni ishara ya mwili ambao Kristo ndiye kichwa. Kwa vyo vyote mwili usio na kichwa hauna uhai. Vivyo hivyo sawa na kanisa ambalo halina msingi juu ya Yesu au kuongozwa naye.

Paulo anaeleza zaidi uhusiano wa kichwa na mwili kwa kusema kuwa kanisa ni ukamilifu wa Kristo. Sisi tumejazwa naye. Kuwepo kwa Kristo duniani ni kwa njia ya kanisa lake. Kanisa lina kazi muhimu katika ufalme wa Mungu. Kila mwamini anapaswa kuwa sehemu ya kazi ya kanisa.

## KULIFUNDISHA SOMO

### Utangulizi

Uliza: "Ina maana gani kuitwa shuleni? Mwalimu mkuu ameyaona matokeo yako na anataka uwe mwanafunzi katika shule yake.

"Kwa njia nyingine, Kristo anapotuita, wazo ni lile lile. Kristo huwaita wale wanaoamini na wale wawekao tumaini katika yeye. Yeye ni mwalimu mkuu angependa kama tungekuwa wanafunzi katika shule yake. Mtu anayeamini kuwa Kristo hutoa uzima wa milele na uzima ulio tele hujiunga na Kristo na hujifunza njia za Kikristo. Neno, mwanafunzi, lina maana ya anayejifunza.

"Kwa nini wanafunzi, hujiunga na shule? Wengi hutamani kuhitimu, kushinda mitihani na kwenda katika Shule za juu. Katika Shule za juu wanafunzi husoma masomo machache lakini kwa undani zaidi, na yale wanayojifunza huwa magumu zaidi.

"Waamini hufuata Kristo kwa sababu wanaamini kuwa siku moja watarithi uzima wa milele. Wanafunzi hufanya kazi kwa bidii ili wajifunze kutoka kwa Kristo. Imani yao hujaribiwa. Mwanafunzi ambaye amejifunza masomo yake vema, atashinda mtihani wake au majaribu. Lakini yule mwanafunzi ambaye hajajifunza masomo yake vizuri kwa vyo vyote atashindwa mtihani.

"Kwa nini baadhi ya wanafunzi hupenda kujiunga na shule zile nzuri? Wanaamini kuwa tabia nzuri ya shule itawafanya wao wakubalike zaidi katika kupata madaraka na kufahamika.

"Wanafunzi wa Kristo wanayo madaraka makubwa kuliko yote. Roho Mtakatifu hukaa ndani ya kila mwamini na humpa nguvu za kumwimarisha. Biblia inasema Roho Mtakatifu huwafanya wengine waamini ushuhuda wetu kuhusu Kristo."

**Maelezo**

"Tumezungumza maana ya kuitwa na Kristo, ni kupata urithi na kujua nguvu zake. Sasa tumwangalie Kristo kama Kichwa cha Kanisa.

"Kristo ameweza kufanya yote, haya yapite kwa sababu ya kifo chake msalabani. Kifo cha mwanadamu kinaonekana kama mwisho au kushindwa. Kwa sababu Kristo alimtii Babaye, hata mpaka mauti, Mungu alimfufua katika maisha mapya. Baba alimwita Mwanawe kutoka kaburini awe mtawala wa dunia.

"Mungu Baba, alimweka mkono wa kuume kama ishara ya mamlaka na utawala. Alimpa Yesu jina lililo juu ya majina yote, na akaweka vitu vyote chini ya miguu yake. Katika kila ufalme kuna wale ambao hawamtii mfalme, na Mungu aliye Mfalme, atawahukumu watu hao siku moja. Lakini leo huyu Mfalme anatekeleza mpango wake kwa ajili ya utii wa kanisa na kwa kuwaleta watu ili watubu."

**Ukweli Katika Maisha Yetu**

"Juma hili unapoisoma Biblia yako ione kama Bwana akufundisha kitu fulani. Andika yale unayojifunza. Uwe macho unapojaribiwa kuhusu mambo hayo.

"Fahamu kuwa uzima wa milele ni zawadi kubwa kuliko matokeo mazuri ya mtihani. Mshukuru Mungu kwa zawadi hiyo kubwa. Msifu Kristo kwa kuwa shabihu.

"Uwe na hakika kuwa unajishughulisha na kazi ya Mungu kwa njia ya kanisa. Kama hujajitoa kama upasavyo kwa kanisa lako, muombe Mungu akusamehe. Anza kutoa sehemu ya kumi ya vile ulivyonavyo, muda na hata fedha zako."

**Kuomba**

1. Mwombe Bwana ili uwe mwanafunzi wake mzuri, na mwanafunzi mzuri.

2. Omba kuwa Bwana atakupa nguvu kwa njia ya Roho Mtakatifu ili uwe shahidi imara kwake na kumpa utukufu.

SURA YA TISA

# TUMEUMBWA TENA KWA KUSUDI

## KUJITAYARISHA KUFUNDISHA

Somo Kutoka: Warumi 3:9-18

Vifungu vya Leo: Waefeso 2:1-10

**Kifungu cha Kukumbuka**

> "Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani, ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu; wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu" (Waefeso 2:8-9).

Kusudi la Somo Hili: Kuwafundisha wanafunzi wangu kwamba mbinguni ni kama zawadi tu kwetu na sio malipo ya kazi nzuri. Kazi yetu nzuri huonyesha shukrani zetu kwa Mungu kwa ajili ya zawadi yake kwetu.

Vitu vya Kusaidia Kufundisha: Ubao au karatasi kubwa na kalamu.

**Msingi wa Somo Hili**

Kusudi la kifungu hiki linaweza kufupishwa kwa neno, NEEMA. Paulo alisisitiza juu ya neema ya Mungu pamoja na maneno yanayoonyesha wenye dhambi kabla ya neema na mwamini kabla ya kupata neema.

Sasa tuangalie mtu yule aliye nje ya neema katika Waefeso 2:1-3. Paulo anamweleza mtu huyu kama mfu. Mtu mfu hana uhai. Mtu asiye na neema huishi maisha ya kidunia yaliyo chini ya nguvu za Shetani aitwaye mfalme wa hewa. Yeye pia ni mwana asiyetii na ambaye huishi tu kuyatimiza mapenzi yake

kwani yeye ni mchoyo na mlafi. Hufanya lile apendalo kufanya bila kizuizi wala kuwajali wengine. Zaidi ya hayo, yeye ni mwana mwenye ghadhabu. Kila mara huwalipa wale waliomkosea kwa ubaya na chuki. Tena hupata hasira kwa mambo yaliyo madogo.

Wakati fulani pia, kabla ya kuwa waamini kwa neema ya Mungu kwa njia ya Yesu Kristo, sisi nasi tulikuwa kama huyu mtu hata ingawaje hatukutenda kama yeye. Mtu huyu (kama sisi tulivyokuwa) amepotea pasipo Mungu.

Paulo hakusimama hapo. Katika kifungu cha nne, anatupa tumaini. Anaanza na neno, lakini. Neno, lakini, linatueleza ya kuwa kuna mabadiliko yanayofuata. Ingawaje tu wafu katika dhambi zetu, kuna kitu Mungu alichofanya cha kutusaidia.

Mungu akiwa mwingi wa rehema, kwa sababu ya upendo wake mwingi ingawaje tulikuwa wafu katika makosa yetu na dhambi, alitufanya sisi hai pamoja na Kristo. Kwa neema tumeokolewa.

Neema ni kipawa cha ajabu ambacho sisi hatustahili. Neema ni baraka ambayo sisi hatustahili. Ni tendo la mtu mmoja. Mtoaji peke yake ndiye anayehusika. Mpokeaji hastahili wala haombi.

Mungu ametenda yale ambao hakuna mwanadamu awezaye. Mungu ametupa maisha mapya kwa njia ya Yesu. Hilo ni tendo la Mungu, lake Mungu mwenyewe! Hakuna mtu awezaye kuwa mkamilifu kiasi cha kumpendeza Mungu, kwa hivyo, Mungu alimtoa Mwanawe mkamilifu mahali petu sisi. Hii ndiyo ajabu ya upendo wa Mungu.

Neema ya Mungu ni ya ajabu kwetu sisi tunaomwamini, lakini Paulo anaeleza matokeo ya neema. Katika kifungu cha 6 na 7 tunaambiwa kuwa tumefufuka pamoja na Kristo na tumekaa pamoja naye katika ulimwengu wa roho. Tumeketi

Kikundi kingine kisome vifungu vya 5 na 6 na watoe maelezo katika karatasi zao kuhusu anayezungumzwa katika vifungu hivi.

Kila kikundi kisome orodha yake kwa kikundi chake. Waulize wanafunzi kama wameona tofauti katika watu walioelezwa. Waambie wasome kifungu cha 4 kwa sauti pamoja.

Waulize ni kwa jinsi gani tofauti kubwa kama hiyo imekuwepo? Ni nani anayehusika na tofauti hizo?

Waulize wanafunzi wangependa wawe kama mtu gani?

Waambie wasome vifungu vya 8 na 9 na watafute ni kwa jinsi gani wanaweza kuwa kama mtu yule aliyeelezwa katika vifungu vya 5 na 6.

**Maelezo**

Waambie wanafunzi waangalie vifungu vya 1-3, na waelewe kuwa vifungu hivi vinatueleza sisi sote kabla ya kumpokea Kristo. Hivi ndivyo tulivyokuwa mbele za Mungu pasipo imani katika Kristo.

Kama wanafunzi wanavyoelewa kuwa sisi sote ni wenye dhambi, ni lazima wawe na subira kwa wale ndugu na wenzao darasani ambao hawajampokea Kristo bado. Kwa maneno mengine tusijione sisi ni wenye haki. Jambo jingine la kuwakumbusha ni kuwa, ni njia ya kipawa cha neema ya Mungu tu mwanadamu aweza kuokolewa. Hakuna hata mmoja anayeweza kununua njia ya kwenda mbinguni. Matendo mema yawe ya kumwonyesha Mungu shukrani zetu kwa neema yake kwetu.

**Ukweli Katika Maisha Yetu**

Tunapoishi katika maisha haya tutakutana na watu wengi ambao hawamfahamu Bwana wetu, nao wanaishi kama wale

katika ufalme wa Mungu sasa. Hatuvitazami vitu kwa mwenendo wa dunia, lakini sasa kwa kuwa tumeketi katika ulimwengu wa roho tumeviona vitu jinsi Mungu anavyoviona. Tena, tumekubalika mbele za uso wa Mungu sasa. Tunaweza kuingia katika mlango wa mbinguni na kuwa na ushirika na Mungu sasa kwa njia ya maombi. Kwa kuwa sasa tupo katika ufalme wa Mungu, tunaye mfalme mpya. Yesu anatawala kama mfalme wetu. Yeye amesimama kwa ajili ya kujitoa kwetu, kuabudu na kumtii. Tumeyaweka mbali mapenzi yetu ya zamani ya kuwatumikia wengine, na sasa tunamtumikia Kristo. Hali hii ya mabadiliko ni ya maisha yetu yote na tunaiita kujikana mwenyewe.

Kwa nini Mungu ametenda haya yote? Kifungu cha 7 kinatueleza kuwa Mungu anataka kuonyesha neema yake ya huruma kwetu.

Hakuna hata mmoja wetu anayestahili yote yale Mungu aliyotupa. Ni neema yake tu ndiyo iliyotuokoa.

Vifungu vya 8 na 9 ni vifungu vya msingi. Vinatukumbusha kuwa wokovu hutoka kwa Mungu kama kipawa na kuwa wema wetu peke yake hauwezi kuupata. Mungu hapendi tujivune kwa wema wetu wenyewe bali tujivunie mbele za kila mtu juu ya neema ya ajabu ya Mungu katika Yesu Kristo. Ushuhuda wetu kwa wengine unapaswa kuwa majivuno juu ya upendo mkuu wa Mungu.

## KULIFUNDISHA SOMO

### Utangulizi

Waambie wanafunzi wasome Waefeso 2:1-10. Wagawe katika vikundi viwili. Kipe kila kikundi karatasi na kalamu. Kikundi kimoja kisome vifungu vya 1-3 tena na watoe maelezo ya anayezungumzwa katika vifungu hivyo.

wa vifungu vya 1-3. Sisi Wakristo tunapaswa kuwa macho kuwa hatujioni kama sisi ni bora kuliko wao. Tunapaswa kuelewa kuwa nasi wakati mmoja tulikuwa sawa kama wao mbele za macho ya Mungu.

Tunavyokuwa na kuishi katika Kristo tutatenda matendo mema. Matendo haya ni ya kuonyesha shukrani zetu kwa Mungu kwa ajili ya wokovu wetu. Sio wa kununua. Juma hili mshukuru Mungu kwa kipawa cha neema. Jaribu kumwambia ye yote kuhusu kipawa cha bure cha Mungu cha neema.

**Kuomba**

1. Omba kuwa utakuwa na uwezo wa kuwafundisha wanafunzi wako maana ya neema.

2. Omba kuwa mwanadamu hastahili wokovu kwa kutenda matendo mema.

3. Mwombee ye yote yule katika darasa lako ambaye hajapokea kipawa cha wokovu kutoka kwa Mungu.

SURA YA KUMI

# JAMAA YA MUNGU

## KUJITAYARISHA KUFUNDISHA

Somo Kutoka: Isaya 57:19; Mwanzo 12:2-3

Vifungu vya Leo: Waefeso 2:11-22

**Kifungu cha Kukumbuka**

> "Basi tangu sasa ninyi si wageni wala wapitaji, bali ninyi ni wenyeji pamoja na watakatifu, watu wa nyumbani mwake Mungu" (Waefeso 2:19).

Kusudi la Somo Hili: Kuwafundisha wanafunzi wangu kuwa waamini wote wa mataifa yote ni watoto wa Mungu katika Kristo Yesu.

Vitu vya Kusaidia Kufundisha: Ubao au karatasi na kalamu.

**Msingi wa Somo Hili**

Barua kwa Waefeso imeandikiwa kanisa lililoko Efeso. Ilikusudiwa kusomwa na makanisa mengine vile vile. Kazi kubwa ya umisheni wa Paulo ilikuwa ni kati ya Watu wa Mataifa. Kabla ya kuja kwa Kristo, Watu wa Mataifa walitengwa na Wayahudi. Wayahudi walifikiri kuwa watu wote ambao hawakufuata dini ya Kiyahudi walikuwa najisi na hawakustahili ahadi ya Mungu. Wayahudi walikataa kuwaongoza wengine katika upendo wa Mungu. Walifurahi kuwa watu waliochaguliwa na Mungu. Ahadi ya Mungu kwa Abraham katika Mwanzo 12:2-3 inawahusu watu wengine na siyo Abraham peke yake. Agano linasema kuwa atawabariki watoto wake na hao watakuwa baraka. Pia kwa kupitia hao, jamii zote duniani zitabarikiwa.

Hii ina maana kuwa Wayahudi wangeshiriki baraka zao na wengine. Wayahudi walizificha baraka zote za Mungu kwa ajili yao wenyewe.

Paulo alijua kuwa Mungu alimwita ili awe mmisheni kwa Watu wa Mataifa. Somo la leo linaangalia maana ya kuja kwa Kristo kwa ajili ya Watu wa Mataifa.

Paulo aliwakumbusha Watu wa Mataifa nafasi zao kabla ya Kristo. Andika maneno aliyoyatumia. Alisema waliitwa "wasiotahiriwa" na wale wanaoitwa "waliotahiriwa." Matatizo makubwa yalikuwepo kati ya Wayahudi na Watu wa Mataifa. Wayahudi walishikilia mila ya zamani ya kutahiriwa hata baada ya kupokea agano la Mungu katika Yesu Kristo. Paulo alisisitiza kuwa kutahiriwa ni kwa mwili na hufanywa kwa mikono ya wanadamu, hivyo alikataa kusudi lake katika kuwa Mkristo.

Tena, anashuhudia kuwa mwanzoni watu wa mataifa walikuwa mbali na Kristo na kutengwa na taifa la Israeli. Watu wa Mataifa hawakuwa na tumaini na walikuwa hawajamjua Mungu.

Kama sura ya tisa, badiliko lipo katika neno, lakini. Wakati ule Watu wa Mataifa walipoishi bila matumaini katika maisha na pasipo Mungu, Mungu alifanya kitu cha ajabu. Mungu kwa njia ya Kristo, aliwaleta Watu wa Mataifa katika jamaa yake.

Kristo aliuondoa ukuta kati ya Wayahudi na Watu wa Mataifa na kuviweka vikundi vyote kuwa jamaa moja. Tofauti zilizokuwepo na ambazo bado zipo kati ya Wayahudi na Watu wa Mataifa ni pamoja na ubaguzi wa rangi ambao ni kama tofauti za kikabila, mila, lugha na njia mbalimbali za kuabudu.

Paulo alilieleza tatizo hilo akitumia neno "chuki." Hii ina maana kuwa Wayahudi na Watu wa Mataifa hawakupendana. Hata walichukiana na hawakuzungumzana.

Lakini Kristo aliunganisha makundi haya mawili na kuleta amani. Mapenzi ya Mungu ni kuwa vikundi vyote viwe mwili mmoja katika upendo.

Kifungu cha 17 pia kipo katika Agano la Kale katika kitabu cha Isaya 57:19. Isaya alitabiri kuwa Mungu sio anawapenda Wayahudi tu. Anawapenda watu wote. Hosea pia alihubiri ujumbe kuwa Mungu atawaita wale wasio wake, watu wake. Kwa hivyo Hosea anatupa utabiri mwingine kuwa agano jipya la Mungu halitawahusu Wayahudi tu, bali hata Watu wa Mataifa.

Katika kifungu cha 19 Paulo anatumia lugha kali kuhusu kuwahusiana Watu wa Mataifa. Soma kifungu hicho tena.

Tena Paulo anaeleza kusudi la Mungu la kuwahusisha Watu wa Mataifa katika vifungu vya 20-22. Mungu anatutaka sisi tuwe kanisa lake na makao ya roho wake. Paulo alitumia picha ya jengo. Alisema kuwa msingi ni kama mitume na manabii, naye Kristo ni jiwe la pembeni. Jiwe la pembeni mwa jengo ni imara. Mawe mengine yote yamechongwa ili yawe sawa na jiwe la pembeni. Hii ni kweli hata kwetu. Sisi tumechongwa kwa mfano wa Yesu, ili tujiunge naye katika kanisa lake.

Kanisa lazima liwe hai katika Roho Mtakatifu ili limfuate Kristo kama kichwa.

## KULIFUNDISHA SOMO HILI

**Utangulizi**

Uliza: "Tofauti kati ya Wayahudi na Watu wa Mataifa zilikuwa zipi?" Waambie kuwa Paulo alikuwa Myahudi naye akawa mmisheni kwa Watu wa Mataifa.

Wape karatasi au waorodheshe ubaoni njia zote Paulo aliwaeleza, Watu wa Mataifa kabla hawajamjua Kristo. Jadilianeni orodha hiyo na waambie kila kitu katika orodha

hiyo kina maana gani. Sema: "Andika neno LAKINI," (Kwa herufi kubwa) "na tuangalie ni mambo gani Mungu aliyofanya hata akayabadilisha maisha ya Watu wa Mataifa." Baadaye wanafunzi waorodheshe yale yaliyotokea kwa Watu wa Mataifa baada ya Kristo kujitoa kuwa dhabihu.

**Maelezo**

Wakumbushe wanafunzi kuwa hii ni kweli tu kwa wale wanaomwamini Kristo. Waeleze kuhusu vifungu katika Isaya na Hosea ambavyo vinaeleza kuwa Mungu angewahusisha Watu wa Mataifa katika mpango wake siku moja. Waambie kuhusu ahadi ya Abrahamu na jinsi Wayahudi walivyoshindwa kuitekeleza kwa kuwabariki wengine.

Mungu anao mpango wa kuwapenda watu wote, lakini wakati mwingine tunaenenda kama Wayahudi bila kuwahusisha wengine. Labda wanafunzi wako wanaweza kuwa na mifano mingine kama hiyo. Palikuwepo kikundi cha watu shuleni ambao walikuwa na hakika kuwa wao ni Wakristo waliozaliwa mara ya pili. Lakini wao waliwalaumu wengine kuwa nao si Wakristo kwa sababu hawakuwa wanahudhuria makutano yao. Wanafunzi hawa kama Wayahudi, walikataa kuwahusisha wale ambao walikuwa tofauti nao. Wakati mwingine tofauti za kikabila zinaweza kuleta matatizo katika makanisa. Hata madhehebu mbalimbali hugombana yenyewe kuhusu lipi ni kanisa la kweli. Jambo hili halimpendezi Mungu. Anahitaji amani kati ya wanawe na jamaa yake. Wakristo wasijitenge au kujivunia nafasi zao. Mungu anatupenda sisi sote kwa njia ya neema yake na anatutaka sisi tuwapende wengine. Silika ya mwanadamu haiwezi kupenda kwa njia hiyo, lakini Roho wa Mungu kwa njia ya kanisa anaweza.

**Ukweli Katika Maisha Yetu**

Waulize wanafunzi wajaribu kukumbuka wakati ambao walikataa kumpenda mtu ambaye alikuwa tofauti nao. Je, mtu huyu alitoka eneo, dini, kanisa, kabila au shule tofauti? Waambie wamwombe Mungu awasamehe.

Sema: "Fikiria ni kwa njia zipi ungeweza kuonyesha umoja na amani kwa jamaa ya Mungu katika eneo lako?" Labda wangeweza kuwa na makutano ya vijana na kuwaalika vijana kutoka makanisa mengine wahudhurie.

Waambie wanafunzi wasali na kuomba msaada kwa Mungu ili waweze kuwapenda wengine ambao ni tofauti nao.

**Maombi**

1. Omba kuwa Mungu atakusaidia uwapende wengine kama anavyokupenda wewe. e.

2. Mwombee mshiriki mwingine wa kanisa ambaye wakati fulani hamkuelewana. Omba Mungu akusamehe.

3. Omba kuwa utamkubali kila mwanafunzi kama kipawa cha Mungu kwako.

SURA YA KUMI NA MOJA

# KANISA KATIKA MPANGO WA MILELE

## KUJITAYARISHA KUFUNDISHA

Somo Kutoka: Wakolosai 1:24-29

Vifungu vya Leo: Waefeso 3:1-13

**Kifungu cha Kukumbuka**

> "Ili sasa, kwa njia ya kanisa, hekima ya Mungu iliyo ya namna nyingi ijulikane na falme na mamlaka katika ulimwengu wa roho" (Waefeso 3:10).

Kusudi la Somo Hili: Kuwafundisha wanafunzi wangu kuwa Yesu alikamilisha makusudi ya Mungu ya kumleta mwanadamu kwa Mungu na sasa tunaweza kuomba moja kwa moja kwa Mungu.

Vitu vya Kusaidia Kufundisha: Andika kichwa hiki ubaoni au katika karatasi kubwa.

**Msingi wa Somo Hili**

Paulo anaanza sehemu hii kwa kuwakumbusha Watu wa Mataifa kuwa yeye ndiye aliyekuwa mmisheni kwa ajili ya Watu wa Mataifa. Anasema kuwa Mungu ndiye aliyempa kazi hiyo.

Paulo anaeleza kuhusu siri aliyofunuliwa na Mungu. Siri hii ya ufunuo ipo katika barua zote za Paulo. Aliona kuwa Yesu ni siri kubwa ya ufunuo kwa sababu Mungu ametenda yasiyotegemewa na yasiyowezekana. Mungu amekuwa mtu katika Kristo na zaidi ya haya, Mungu amekufa kwa ajili ya

dhambi za wanadamu. Ni upendo ulio mkuu ambao Mungu ametuonyesha. Tulipokuwa wenye dhambi, na Kristo alitufia.

Paulo alikuwa Myahudi mwenye elimu nyingi ya dini. Aliujua unabii kuhusu Masihi. Hakutegemea kuwa ukamilifu wa unabii huu ungetoka kama ulivyotokea katika Yesu Kristo. Hii ilikuwa siri kubwa kiasi gani kwa Paulo! Hakuwa Myahudi aliyetegemea mambo haya kutimilika. Mungu aliyafanya yakawa siri. Ni kwa njia ya nguvu za Roho Mtakatifu pekee, Pauo aliweza kuielewa siri hii kubwa.

Siri nyingine kutoka kwa Paulo ilikuwa kwamba Mungu angeweza kuwapenda watu wa mataifa kama vile alivyowapenda Wayahudi. Wayahudi hawakuweza kuamini kuwa mbele za Mungu hawakuwa tena watu maalum au wateule. Watu wa mataifa walikuwa sawa nao mbele za Mungu. Yesu alikufa kuwaokoa watu wa mataifa pamoja na Wayahudi. Siri ya mpango wa Mungu ilifichwa kwa sababu Wayahudi wengi hawakuweza kuamini kuwa Masihi atakufa, na kwa vyo vyote kama angekufa, siyo kwa Watu wa Mataifa ili waingie nao katika ufalme wake!

Katika kifungu cha sita Paulo anaieleza siri hii. Watu wa Mataifa ni warithi pamoja nasi, washiriki pamoja nasi katika mwili na wenzetu katika ahadi ya Yesu Kristo. Paulo alieleza kuwa Watu wa Mataifa walio Wakristo ni sawa na Wayahudi walio Wakristo. Mahubiri haya ya ujasiri kuhusu usawa kati ya Wayahudi na Watu wa Mataifa yaliwachukiza Wayahudi kwa kila njia. Wayahudi waliwachukia Watu wa Mataifa. Hawakuweza kula pamoja au kuongea nao, lakini Paulo alieleza kuwa wote walikuwa sawa. Kupigwa kwingi kwa Paulo kulikuwa ni kwa sababu alihubiri kuwa Yesu aliwafanya Watu wa Mataifa sawa. Mwanadamu anaona vigumu kumpenda na kumkubali yule aliyemchukia kwa muda mrefu, lakini Mungu anashiriki mapenzi yake na wale wote wanaomwamini. Watu wa rangi zote na lugha zote na kila

kabila wataingia katika ufalme wa Mungu kama wakimwamini Yesu Kristo.

Paulo aliona kuwa umisheni wake ni kuhubiri siri hii kwa kila mmoja, hata kwa wafalme na wenye mamlaka. Kwa sababu alihubiri ujumbe huu kwa ujasiri kwa watu wote, alipigwa kwa mawe, kwa mjeledi na kufungwa gerezani mara nyingi.

Shida nyingine ambayo Wayahudi walikuwa nayo kuhusu Paulo ni kuwa yeye alifundisha kuwa kwa njia ya Yesu Kristo, mtu anaweza kumwomba Mungu moja kwa moja. (Soma kifungu cha 12.) Wayahudi waliamini kuwa kumwomba Mungu lazima upitie kwa kuhani. Hii iliwafanya makuhani wamchukie kwa sababu kazi yao ingeharibika.

Paulo alisema kuwa katika Kristo, tunao ujasiri na uhakika wa kumfikia Mungu. Mambo ya desturi ni magumu kubadilika, na Wayahudi hawakupenda kuzibadilisha desturi zao juu ya makuhani. Wayahudi walipofuata desturi zao badala ya mpango wa Mungu katika Kristo, Mungu alitenda kazi kwa njia ya Watu wa Mataifa kuieneza injili. Kuna Watu wa Mataifa wengi ambao wametajwa katika Agano Jipya. Timotheo alikuwa nusu Muyahudi na nusu Mtu wa Mataifa.

Wale wanaoshikilia desturi huonyesha majivuno yao na hawamtii Mungu. Kwa sababu aliuelewa uhusiano wake na Mungu, hakujali kupata mateso. Aliweza kushinda vizuizi alivyowekewa na Wayahudi na kumsifu Mungu. Paulo alifahamu kama Kristo alishinda kifo kwa njia ya Roho Mtakatifu, yeye pia atakuwa na nguvu katika kifo. Kwa upande mwingine, Wayahudi waliyaogopa mafundisho ya Paulo. Desturi zao zisizo za maana hazingeweza kuzuia nguvu ya maneno ya Paulo. Matendo yao yalikuwa ni kama ya wanadamu wasio na Mungu. Walitaka kumwua Paulo. Kwa ulinganifu huu, ni rahisi kuona kuwa ukweli wa nguvu za Mungu ni mkubwa kuliko desturi zo zote zile.

## KULIFUNDISHA SOMO HILI

**Utangulizi**

Waambie wanafunzi wasome vifungu hivi na wahesabu ni mara ngapi neno siri au mpango wa siri limetumika. Waambie wajaribu kueleza maana ya neno, siri. Siri ni kitu ambacho hakifahamiki au kueleweka. Sema: "Ubaguzi wa rangi ni kitu gani? Ni kumchukia mtu kwa sababu yeye ni tofauti. Labda ni rangi ya ngozi yake, desturi au kabila ambavyo vinamfanya awe tofauti." Uliza: "Je, umeona ubaguzi wo wote wa rangi?"

**Maelezo**

Kristo alivunja vizuizi ili Wakristo wapendane na kuwakubali Wakristo wenzao kama sawa. Kwa Mungu, hakuna tofauti ya rangi, kabila, desturi, elimu, mume au mke. Ye yote yule ambaye hautimizi usawa huu katika jamaa ya Mungu anafanya dhambi kwa Mungu. Yesu alielewa vishawishi vya watu wengine kujiona bora kuliko wengine hasa matajiri. Alisema kuwa ni rahisi kwa ngamia kuingia katika tundu la sindano kuliko kwa mtu tajiri kuingia katika ufalme wa Mungu.

Kuna tatizo bado kati ya wanaume na wanawake. Wanaume wengi wanajiona kuwa wao ni bora kuliko wanawake. Biblia haitufundishi jambo hilo. Biblia inatufundisha kuwa kila mmoja anayo kazi ya kufanya, na kila kazi ni muhimu. Wazo la Mungu la usawa sio kati ya wanaume tu, lakini pia linawahusu wanawake. Katika kanisa wanaume kwa wake lazima wafanye kazi bega kwa bega.

**Ukweli Katika Maisha Yetu**

Sema: "Nielezeni tena maana ya neno siri. Habari njema ni siri pia leo. Watu ambao hawamfahamu Yesu hawawezi kuuelewa mpango wa Mungu wa kumwokoa mwanadamu. Wakristo wanapaswa kuwa kama Paulo na kuieleza siri hii ya

ajabu kwa wengine." Wanafunzi wawafikirie marafiki ambao hawamfahamu Yesu na wamwombe Mungu ili waweze kushiriki siri hii ya upendo wake nao.

"Wakristo hawawezi kuwa kama Wayahudi kwa kuzificha habari njema za Kristo wao wenyewe."

**Kuomba**

1. Omba ili Mungu akusaidie uweze kushiriki siri za Yesu na wanafunzi wako.

2. Omba ili wanafunzi waelewe kuwa ubaguzi ni dhambi kwa Mungu.

SURA YA KUMI NA MBILI

# MAOMBI YA PAULO KWA KANISA

## KUJITAYARISHA KUFUNDISHA

Somo Kutoka: Wafilipi 1:8-14; Yohana 16:23-24

Vifungu vya Leo: Waefeso 3:14-21

**Kifungu cha Kukumbuka**

> "Awajalieni, kwa kadiri ya utajiri wa utukufu wake, kufanywa imara kwa nguvu, kwa kazi ya Roho wake, katika utu wa ndani" (Waefeso 3:16).

Kusudi la Somo Hili: Kuwafundisha wanafunzi wangu kuwa kwa njia ya sala wanaweza kushinda matatizo kwa msaada wa Roho Mtakatifu.

Vitu vya Kusaidia Kufundisha: Karatasi na kalamu kwa kila mwanafunzi.

**Msingi wa Somo Hili**

Paulo anaamuru maandiko haya kwa maneno yale yale ya sura ya kumi na moja! Kwa sababu hiyo, tunakumbushwa sababu hiyo ilikuwa ipi tunapoangalia tena Waefeso 2. Mtakumbuka, sura ya pili imegawanywa katika sehemu mbili. Sehemu ya kwanza ni vifungu vya 1-10 ambao ni ujumbe wa ujumla kwa mwanadamu aliyepotea, pamoja na kipawa cha neema ya Mungu na matokeo ya neema ile. Sehemu ya pili ni vifungu vya 11-22 ni kuhusu Watu wa Mataifa walivyokuwa kabla ya Kristo, na yale Mungu aliyotenda kwa njia ya Kristo na matokeo ya kumfahamu Kristo. Ujumbe mkuu ni kuwa ingawa mwanadamu alipotea, Mungu kwa njia ya Yesu

amefanya mabadiliko, na matokeo yake ni uzima mpya na wa milele.

Paulo aliposema, "Kwa sababu hiyo..." alikuwa na maana ya kazi Mungu aliyoifanya kwa mwanadamu, yaani wokovu. Paulo anasema kwa kuwa Mungu alitendo tendo la kumwokoa mwanadamu, atamwomba Mungu ili awape Watu wa Mataifa nguvu kwa njia ya roho wake ili wawe imara. Paulo alifahamu kuwa kwa njia ya Yesu angeweza kuomba moja kwa moja kwa Baba kwa ujasiri na kuwaombea wengine. Paulo alikuwa mwangalifu kwani aliomba tu vile vitu ambavyo vilikuwa katika mapenzi ya Mungu. Mungu anapenda kila mmoja wa watoto wake kuwa na Roho wake.

Paulo aliomba ili makao ya Kristo yawe katika mioyo ya Watu wa Mataifa kwa njia ya imani. Haya pia ni mapenzi ya Mungu. Sala zetu zote zinapaswa kuwa sawa na mapenzi ya Mungu.

Katika kifungu cha 17, Paulo anaeleza kuhusu mizizi. Mizizi ina kazi nyingi katika mmea. Mizizi hulisha mmea ili uweze kukua. Vivyo hivyo, kukua kwetu Kikristo lazima kutokane na upendo kwa Mungu na kwa Wakristo wenzetu. Pili, mizizi husaidia mimea iwe imara ardhini tena huizuia isipeperushwe na upepo. Kwa njia nyingi mizizi ndio nguvu ya mmea. Sisi, pia, lazima tuwe na msingi wa upendo ili tuweze kuyashinda majaribu na shida bila kumwacha Kristo.

Katika kifungu cha 18 Paulo anaeleza kuwa ni vigumu kuelewa upendo wa Mungu. Anasema kuwa tunahitaji nguvu za Mungu ili tuweze kueleza jinsi upendo wa Kristo ulivyo mkuu. Anatutaka tuuelewe upendo wa Kristo, pia ametutahadharisha kuwa hatutaweza kuufahamu kikamilifu. Paulo anasema kuwa haiwezekani kuufahamu upendo wa Mungu bila Roho Mtakatifu, naye Roho Mtakatifu huja tunapompokea Kristo. Kwa hivyo wale ambao hawamwamini Kristo hawawezi kuufahamu upendo wa Mungu.

Paulo anasema kuwa kama tungeweza kuufahamu na kuuelewa upendo wa Kristo, tungejazwa kabisa na Roho wa Mungu. Paulo anaeleza kuwa hali yote ya Mungu inatokana na upendo wake kwetu. Mungu haivumilii dhambi kwani yeye anatupenda sisi, nayo dhambi inatuharibu sisi. Wazazi walio wengi hawataruhusu watoto wao waendelee kutenda mambo mabaya kama kuwapiga watoto wengine. Badala yake, kwa sababu wanampenda mtoto, watamfundisha nidhamu kwa manufaa yake mwenyewe. Matendo yote ya Mungu kwetu yanatokana na upendo wake. Paulo anaeleza kuwa kama tungeweza kujua na kuelewa upendo huo, tungekuwa kama Kristo, kwa sababu, tungeamini mapenzi ya Mungu kwa moyo wote kama Kristo alivyofanya.

Paulo anamalizia kuhusu wokovu na kukua kwetu katika kifungu cha 20. Kwake yeye, Kristo katika kutenda kazi yake ndani yetu, kumetupa ufunguo kwa maisha yetu ya Kikristo. Kristo anaishi ndani yetu na kufanya kazi ndani yetu kwa njia ya Roho wake ili ayabadilishe maisha yetu ya ndani. Mwanadamu amejaribu tena na tena kubadilisha tabia yake, lakini kila mara ameshindwa. Jela mara nyingi haziwezi kuwabadilisha wafungwa mpaka wamfahamu Yesu.

Wakati mwingine watu wanajaribu bila mafanikio kutenda kama Wakristo bila kumpokea Yesu. Kristo lazima awe anaishi ndani ya mtu ili aweze kubadilika na kuwa kama Kristo. Mwanadamu huamua kila siku kumruhusu Mungu ayatawale maisha yake anapoomba, anaposoma Biblia na anapomtii Mungu.

Mwishoni Paulo anatukumbusha kuhusu nguvu za Mungu ili tutende zaidi kuliko tunavyoweza kuomba au kufikiria. Mungu anafanya kazi katika maisha yetu akitubadilisha kwa ajili ya utukufu wake.

## KULIFUNDISHA SOMO HILI

**Utangulizi**

Mpe kila mwanafunzi karatasi pamoja na kalamu. Waambie waandike maana ya maombi. Wasome ujumbe huo wa maandiko na waorodheshe maombi ya Paulo. Waulize wanafunzi kama maombi ya Paulo yalikuwa ni kwa mapenzi ya Mungu. Uliza: "Je, Mungu alipendelea vitu vile Paulo alivyoviombea?" (Ndiyo) "Basi Paulo aliomba kwa mapenzi ya Mungu. Sasa orodhesha baadhi ya vitu ambavyo wangeweza kuviombea wakati wo wote wakijua ya kuwa ni kwa mapenzi ya Mungu."

Sema: "Sasa andika maana ya upendo. Waeleze kwa nini wamejifunza juu ya upendo wa Mungu."

**Maelezo**

Mungu alichagua kuonyesha mpango wake wa siri wa wokovu, kwa njia ya Kristo ili kuleta utukufu katika jina lake. Kwa njia yake tunaweza kuelewa kwa kiasi ukuu wa upendo wa Mungu. Mungu ni wa ajabu, mwenye upendo usio na kikomo. Upendo wa Mungu ni mkuu hivyo kuwa hatuwezi kuufahamu bila Roho wake kutufundisha sisi.

Mungu alichagua kanisa kama chombo chake cha upendo kwa ulimwengu. Kristo alifufuka kutoka kwa wafu na akarudi mbinguni. Sasa kanisa likiwa limejawa na Roho wake, ni mwili wake hapa duniani. Kanisa linapaswa kuonyesha upendo wa Mungu ulimwenguni. Sisi ambao ni kanisa twapaswa tumletee Mungu utukufu. Tunapaswa kuonyesha ulimwengu kweli Mungu ni nani. Ni lazima tuonyeshe upendo ule mkuu ambao yeye alitupenda kwao.

**Ukweli Katika Maisha Yetu**

Waambie wanafunzi wazifikirie njia ambazo wanaweza kuonyesha upendo wa Mungu kwa rafiki zao ambao hawamfahamu Kristo.

Waambie waorodheshe vitu katika Biblia ambavyo wangewaombea wengine au wao wenyewe ili waelewe kuwa ni mapenzi ya Mungu. Wahimize watumie maandiko katika maombi yao.

**Kuomba**

1. Omba kuwa utaweza kuonyesha upendo wa Mungu kwa wanafunzi wake.

2. Tafuta kifungu cha maandiko ambacho ungetumia kumwombea kila mwanafunzi wako juma hili. Waambie ni kifungu kipi ambacho umewachagulia. Ujumbe huo unayo mawazo mazuri.

SURA YA KUMI NA TATU

# TUKUE KWA MFANO WA YESU

## KUJITAYARISHA KUFUNDISHA

Somo Kutoka: Wafilipi 2:12-13; Waefeso 5:15-17; Wathesalonike 2:12

Vifungu vya Leo: Waefeso 4:1-16

**Kifungu cha Kukumbuka**

> "...Mwenende kamą inavyoustahili wito wenu mlioitiwa" (Waefeso 4:1).

Kusudi la Somo Hili: Kuwafundisha wanafunzi wangu kuwa wanapaswa wakue zaidi kama Kristo kila siku.

Vitu vya Kusaidia Kufundisha: Andika hicho kichwa ubaoni.

**Msingi wa Somo Hili**

Katika sura ya kumi na mbili tumejifunza juu ya upendo mkuu wa Mungu. Tumejifunza kuwa alionyesha upendo wake mkuu kwa kumtoa Yesu afe badala yetu. Tumejifunza leo kuwa kanisa lazima lionyeshe upendo wa Mungu kwa dunia ambayo haiwezi kufahamu upendo huo.

Katika habari hii Paulo ameweka njia kamili ambazo sisi Wakristo twaweza kuzitumia kuonyesha upendo wa Mungu. Paulo aliwataka watu wa Efeso waishi maisha ambayo ni sawa na wito wao waliowekewa na Mungu alipowaita. Mungu humwita kila mtu kwa njia ya Kristo. Yesu alisema kuwa hakuna awezaye kwenda kwa Baba bila kupitia kwake. Kiwango cha Mungu ni kikamilifu. Paulo ametutaka tujitoe kwa Kristo na kumruhusu Roho wake atukamilishe.

Katika Wafilipi 2:12-13 Paulo anatukumbusha tutimize wokovu wetu kwa kuogopa na kutetemeka kwa sababu Mungu anatenda kazi ndani yetu ili atufanye tuweze kumtii yeye.

Katika kutimiza wokovu wetu mambo mawili yanahusika, Mungu akitenda kazi ndani yetu na matendo yetu yataonyesha kuwa tunatii uongozi wake. Hebu tuangalie mfano wa msichana mdogo kabla ya kuolewa. Hufanya yale ambao apendayo kufanya na huwatembelea rafiki anapopenda. Kwa vyo vyote baada ya ndoa mambo hubadilika. Hufanya mambo karibu yote na mume wake tena hupenda kukaa naye anapotoka kazini. Hupika na hufanya yale yanayompendeza. Mwanamke mzuri hufurahi anapofanya mambo haya kwa sababu anampenda mumewe.

Matendo ya yule msichana hubadilika kwa sababu sasa ameolewa. Tena mambo anayotenda ni tofauti kwa sababu anampenda mumewe.

Hata kwa Mkristo mabadiliko kama hayo ya matendo hutokea. Kwanza humpokea Kristo na kuunganishwa na Kristo. Baadaye huenenda tofauti kwa sababu anampenda Kristo. Katika vifungu hivi Paulo anatueleza yale yanayompendeza Bwana. Kwa moyo mkunjufu tunapaswa kuyatenda mambo haya ili tumfurahishe Kristo kwani tunampenda na tunamshukuru kwa yale aliyotutendea.

Paulo aliwataka watu wa Efeso wawe wanyenyekevu, waungwana na wavumilivu. Huu ndio mwenendo unaompendeza Bwana. Mtoto tangu akiwa mdogo hufundishwa mambo yale yanayokubalika katika jamii anayoishi. Hujifunza mambo hayo na kuyatenda wakati wote wa maisha yake. Ni vivyo hivyo ilivyo kwa maisha ya Mkristo. Tunajifunza ni mwenendo gani utakaomfurahisha Baba, ili tuweze kuishi hivyo. Paulo alieleza baadhi ya mambo haya.

Katika kifungu cha 2 Paulo anasema kuwa tunapaswa kuonyesha upendo kwa kuwavumilia wengine. Kama mtu anao uvumilivu basi atawavumilia hata wengine. Pia tuwe na umoja katika mwili wa Kristo. Yaani tufanye kazi pamoja katika Jamaa ya Mungu. Kuwavumilia wengine na kuwa na umoja siyo kitu cha kawaida kwa wanadamu. Dunia yetu leo ni mfano dhahiri wa mafarakano na ugomvi kwa sababu ya kukosa kuaminiana na chuki. Mkristo mpya hujifunza mwenendo mwema kwa matendo.

Paulo alieleza kuwa umoja ni wa lazima kwa sababu ya umoja wetu katika Mungu. Katika kifungu cha 7 Paulo anawataka Wakristo watumie kipawa maalum Mungu alichowapa. Kila Mkristo anao wajibu maalum wa kazi maalum katika Jamaa ya Mungu. Katika 1 Wakorintho 12-14, Paulo alieleza tatizo la yule anayeitaka karama ya mtu mwingine, kujivunia karama tulizopewa kwa wivu. Paulo aliwataka Wakorintho wawajibike kwa Mungu kwa karama zao. Paulo alisisitiza kuwa karama hizo zimetolewa kwa kusudi moja katika kujenga mwili wa Kristo. Kwani kwa Jamaa yo yote kuishi kwa amani ni lazima washiriki wa Jamii wawe na kazi na kufanya kazi pamoja. Paulo anasema kuwa tunapaswa kuzitumia karama zetu ili tuweze kukomaa. Kukomaa huku ni pamoja na kufikia kimo cha Kristo. Mtoto tangu anapozaliwa mpaka anapokufa, bado yupo katika kukomaa. Mtoto hujifunza kufanya mambo kwa njia fulani, naye huwaiga wakubwa zake. Kwa njia hiyo hiyo tunamwiga Kristo na kujifunza njia ambazo Mkristo angeishi. Ikiwa bado tutabakia kama watoto wadogo na kujipenda tu, basi tungekuwa katika hatari ya kudanganywa na watu waovu na waongo. Paulo anasema kuwa Wakristo wanapaswa kukua ili wawe watu waliokomaa. Alikuwa na maana kuwa watajifunza kuyatenda yale mafundisho ya Yesu kwa njia ya Neno lake na Roho wake.

## KULIFUNDISHA SOMO HILI

**Utangulizi**

Sema: "Soma kifungu cha 2 na orodhesha maadili 3 ambayo Wakristo wanapaswa kuyatenda." (kuwa wanyenyekevu, watulivu na wavumilivu) Waambie wanafunzi waeleze maana ya kila neno. Mwulize mmoja aeleze tofauti katika mwenendo wa mtu aliyeoa na yule ambaye hajaoa. Linganisha mabadiliko ya kazi na mabadiliko ya mwenendo kwa maisha mapya aliyoyapata mtu anapompokea Kristo. Maisha yake huwa tofauti.

Uliza: "Kuna tofauti gani katika mwenendo kati ya wale walio Wakristo na wale wasio Wakristo?"

Uliza: "Ni tofauti zipi katika mwenendo zilizopo kati ya mtoto na mtu mzima? Pia tulinganishe mwenendo wa Mkristo mpya na yule wa miaka mingi."

**Maelezo**

Mungu yumo ndani yetu akifanya kazi ya kutubadilisha na kutufanya tuwe kama Kristo kila siku. Kama vile mzazi afundishavyo mtoto, mtoto naye anapaswa kushiriki katika kujifunza.

Wakristo wanapaswa kuenenda mwenendo wa Kristo ili waweze kukomaa. Kristo anatenda kazi ndani ya maisha yetu kwa njia ya Roho wake akitufundisha na kutufunza. Kwa sababu tunampenda Mungu, tunashirikiana naye kwa kumtii. Yakobo alisema kama unamwamini Mungu, utatenda yaliyo mema kwa jina la Yesu. Yesu alisema kuwa yale ayafanyayo yeye, watoto wake pia watayafanya, tena watafanya hata yaliyo makubwa zaidi.

**Ukweli Katika Maisha Yetu**

Sisitiza umuhimu wa kuisoma Biblia kila siku. Waambie wanafunzi waombe kabla ya kulisoma Neno la Mungu juma

hili. Wamwombe Bwana ili awape somo maalum kila siku. Waambie waweke orodha ya masomo haya na waorodheshe njia waliyojifunza hilo somo ili waweze kujifunza vizuri zaidi. Waambie wachunguze kama jitihada yao hii ya kulisoma Neno la Mungu inawaletea tofauti katika kuisoma Biblia kwa njia yo yote ile.

**Kuomba**

1. Mwombe Mungu akufundishe juma hili.
2. Omba kuwa utakuwa kama Kristo. Mwombe Mungu akuongoze ili uweze kuwaongoza wanafunzi wako kuwa kama yeye.